www.umg.co.tz
*Leo yetu ndiyo kesho yetu*
# Mwelekeo
Toleo Na. 00003
| Jumatano Machi 01 - Machi 07, 2023 |
umgdigital · umgdigital · mwelekeo@umg · umgdigital



MAKALA
**Samia aweka historia ujenzi wa madarasa**
Habari ⇉ Uk.10




SIASA
UK.14

UCHUMI
**Bwawa la Nyerere zaidi ya mradi**
Nambari wani Afrika Mashariki, Afrika wa nne
Uk. 12



HABARI NDANI

**Kina cha maji Bwawa la Nyerere chafikia mita 134.39**
Uk. 7



**Zijue dalili za tezi dume na tiba yake**
MAKALA UK.12

⇉ Uk. 24



Kocha Mgunda amzungumzia Kibu Denis

# Neema yawashukia vijana 22,000
Uk. 4

- Ni waliokwama kuingia kidato cha 1
- Wamo kidato cha nne wa Div. 0




## 'Daladala wakikupandishia nauli, piga 0800110019'
Uk. 4

# Dk. Mwinyi aahidi neema kilimo cha mboga Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imeahidi kuimarisha kilimo cha mbogamboga na matunda visiwani humu ili kutosheleza mahitaji ya wananchi na kuuza nje ya nchi.

Akifungua kituo maalum cha kuhamasisha kilimo hicho hivi karibuni, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (pichani), alisema serikali yake itaweka mazingira wezeshi ya kuimarisha kilimo hicho.

"Pamoja na kuweka miundombinu itakayosaidia kukuza kilimo hicho, tutaweka mazingira yatakayosaidia kushamiri visiwani.

"Kuimarishwa kwa kilimo hicho kutasaidia kukidhi mahitaji ya ndani na pia kuuza nje ya nchi ambako kuna soko kubwa litakalosaidia kuingiza fedha za kigeni," alisisitiza Dk. Mwinyi na kuongeza:

"Kilimo cha mbogamboga, ni moja ya vipaumbele vyetu kutokana na umuhimu wake kwa uchumi wetu, hivyo tutaweka mazingira mazuri yatakayosaidia kuongeza uzalishaji kufikia masoko ya uhakika na kuweka miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, utafiti na wataalam wa ugani watakaowasaidia wakulima wetu."

Dk. Mwinyi alisema mipango ya kujenga kituo cha kisasa cha kuhifadhi mbogamboga na matunda yanayosafirishwa nje katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume, imekamilika.

Aliongeza kuwa pia mipango ya kujenga vituo hivyo katika Bandari ya Zanzibar na bandari nyingine visiwani humu, ipo mbioni kukamilika ili kuhifadhi mazao hayo yanayoharibika haraka kutokana na hali ya hewa ya joto. Alisisitiza kuwa soko la mazao yanayotokana na kilimo hicho, ni kubwa visiwani humu kwa kuwa asilimia 90 ya mbogamboga na matunda zinatumika kwa soko la ndani katika hoteli zaidi ya 600 zinazohudumia watalii zaidi ya 500,000 wanaotembelea visiwa hivi kila mwaka.



> **Kilimo cha mbogamboga, ni moja ya vipaumbele vyetu kutokana na umuhimu wake kwa uchumi wetu....**

Rais Dk. Mwinyi alipongeza Chama cha Wakulima wa Mbogamboga, Matunda na Maua nchini (TAHA) kwa jitihada inazofanya kukiendeleza kilimo hicho visiwani humu kwa zaidi ya miaka 10.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inatambua na kushukuru mchango mkubwa wa TAHA katika kuhamasisha na kukiendeleza kilimo cha mbogamboga na matunda visiwani ambacho kimesaidia kutoa ajira kwa makundi ya vijana na wanawake mbali ya kuimarisha lishe na kusaidia kuongeza pato la wakulima wadogo Zanzibar," alisisitiza Rais Dk. Mwinyi.

Akizungumza katika uzinduzi wa kituo hicho, Afisa Mtendaji Mkuu wa TAHA, Jacqueline Mkindi, alisema chama hicho kimekuwa kikishirikiana na wadau mbalimbali visiwani humu.

Kwa mujibu wa Mkindi, matokeo ya jitihada hizo ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa mazao hayo na kupunguza uagizaji wa mazao hayo kutoka nje kutoka asilimia 80 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 26 mwaka 2021.

"Katika kipindi hicho, tumetengeneza mfumo wa kufikia masoko ya ndani na nje ambako wakulima 8,000 wamenufaika na mfumo huo," alisisitiza Afisa Mtendaji Mkuu huyo. Kituo hicho cha kisasa kimejengwa na TAHA kwa ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (EU) na Finlad – FFD.

## TANAPA kufanya makubwa miaka 50 Hifadhi Ml. K`njaro

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limeandaa shughuli mbalimbali za kijamii katika kuadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro.

Hifadhi hiyo ambayo ni moja ya vivutio vya vinavyotambuliwa kama sehemu ya urithi wa dunia, ndipo ulipo mlima mrefu zaidi barani Afrika, Mlima Kilimanjaro.

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa utalii na uhifadhi, TANAPA imepanga kufanya shughuli mbalimbali za kijamii katika maadhmisho hayo ikiwa ni pamoja na kupanda miti katika hifadhi hiyo na kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii zinazoizunguka.

Akizungumzia maadhimisho hayo, Naibu Kamishna Uhifadhi wa shirika hilo, Herman Batiho, alisema yatakamilishwa kwa kikao cha wadau wa utalii na uhifadhi.

"Tutakamilisha maadhimisho ya miaka 50 ya Hifadhi ya Mlima Kilimajaro kwa kufanya kikao cha wadau wa utalii na uhifadhi ambapo tutaangalia tulipotoka, tulipo na changamoto zinazokabili hifadhi hiyo na uhifadhi kwa ujumla," alifafanua Batiho.

Aliongeza: "Tutaangalia na kujadili mafanikio ya hifadhi hiyo hasa Mlima Kilimanjaro kwa miaka 50 iliyopita na pia tutaangalia Mlima huo utakavyokuwa miaka 50 ijayo na tutakuwa na maazimio ya nini kifanyike ili kulinda."

Hifadhi hiyo ni moja ya vivutio vinavyotembelewa na wageni wa ndani na nje ambao hupanda Mlima Kilimanjaro wenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari.

# Wapendekeza polisi wafungwe kamera

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya wadau wa habari, wamependekeza askari wa Jeshi la Polisi nchini, wafungwe kamera kuzuia ukiukaji wa haki za binadamu wakati wa ukamataji na kumhoji mtuhumiwa.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alitoa pendekezo hilo wiki iliyopita jijini Dar es Salaam baada ya kuwasilisha maoni yake kwenye Tume ya Rais ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini.

Balile alisema askari wakifungwa kamera, watajiepusha na tuhuma za kubambikia raia kesi au kuwanyanyasa wawapo mikononi mwao. Alisema TEF imependekeza kuwa Polisi iangaliwe kuanzia ukamataji wa mtuhumiwa, upelelezi hadi kufunguliwa kwa mashitaka. Balile alisema wananchi wengi hulalamika kubambikiwa kesi polisi na katika Ofisi ya Mwendesha Mashtaka ya Taifa. "Askari kama Marekani, wote wanavaa kamera kwa hiyo ukilalamika, wanarudi kwenye mfumo kuangalia kwa sababu kamera zinarekodi mazungumzo yote," alisema. Alisema TEF imependekeza kuwa Majeshi ya Polisi na Magereza na Tume ya Kudhibiti na Kuzuia Dawa za Kulevya, visimamiwe na Kamishna raia ambaye atatoa ripoti ya utendaji wa vyombo hivyo kila mwezi.

### RWAMBOW ALIA NA POLISI

Kwa upande wake, Kamanda na Kachero mstaafu wa Jeshi la Polisi (SACP), Jamal Rwambow (picha ndogo), alipendekeza marekebisho ya sheria ili maelezo ya awali anayotoa mtuhumiwa kituo cha polisi, yasitumike kama ushahidi mahakamini. Alisema mtuhumiwa anaweza kutoa maelezo ya awali polisi katika mazingira magumu pale anapokutana na askari wasio na uadilifu ambayo yanaweza kumtia hatiani mahakamani.

"Nimewaambia hiyo inaweza kuwa chanzo cha malalamiko mengi maana baadhi ya wapelelezi wasio na uadilifu, wanatumia njia zisizo halali kupata maelezo… nimewaambia wajaribu kuangalia ungamo lilipatikanaje," alisema.

Wahadhiri wa vyuo vikuu, wametaka watumishi wanaofanya kazi katika Taasisi za Haki Jinai kuundiwa chombo cha



kuwachunguza ili pale maofisa hao wanapokiuka maadili wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhadhiri Aman Mwakolo, kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mbeya (CUCOM), alisema kuundwa kwa chombo hicho kutaondoa upendeleo pale wapelelezi wanapokiuka maadili.

Alitoa mfano kuwa maofisa wa TAKUKURU, wanapobainika kujihusisha na rushwa wamekuwa wakipelekwa kwenye baraza la nidhamu jambo alilosema linaleta upendeleo. "Na wenyewe pia ni binadamu kuna uwezekano kabisa kwamba wakampendelea… ikitokea mtu wa TAKUKURU ametenda kosa la masuala ya rushwa wao wanashughulikia sana makosa ya kinidhamu na siyo kufikishwa mahakamani kama watuhumiwa wengine wa makosa ya rushwa," alisema. Mhadhiri wa Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idd Mandi, alisema wamependekeza iundwe tume ya kusimamia maadili ya jeshi la polisi ambayo pamoja na mambo mengine, itapokea malalamiko ya wananchi na kuchukua hatua.

Alipendekeza pia sheria ya dhamana irekebishwe na kuongeza makosa ya kudhaminiwa ili kupunguza msongamano magereza. Naye Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kaspar Mmuya, alipendekeza wafungwa wenye makosa madogo madogo wapewe zaidi adhabu mbadala badala ya kifungo ili kupunguza msongamano magerezani. Mmuya alipendekeza kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Parole apewe mamlaka ya mwisho ya kuamua idadi ya wafungwa wakutolewa na mfumo huo badala ya inavyoamuliwa sasa na Waziri wa Mambo ya Ndani.

Tume ya Rais ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini kwa sasa iko mikoani kupokea maoni ya wananchi ili ije na majibu ya njia bora za upatikanaji wa haki nchini. Wiki iliyopita, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu Othman Chande, alikaririwa akieleza kuwa ziara hiyo itawafikia wafungwa na mahabusu, askari wa vyeo vya chini, makazi ya polisi na askari magereza, asasi za kiraia pamoja na watu wa kada mbalimbali. Hadi sasa, maofisa wa juu wastaafu Jeshi la Polisi, Magereza, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Mkemia Mkuu na Mganga Mkuu wa Serikali, vyuo vikuu na asasi za kiraia, wameshawasilisha maoni kwenye tume hiyo jijini Dar es Salaam. Aidha, Jaji Chande, alisema wanatarajia kuhojiana moja kwa moja na wafungwa na mahabusu ndani ya magereza 14 makuu na madogo.

"Tumeelekeza mamlaka husika Magereza na Polisi wasiandae, tunataka tukute hali kama ilivyo," alisema.

RIPOTI MAALUM KUTOKA NANYUMBU



Vikongwe Sigele Mtehiya (90) na mumewe, Laisa Mmole (97), wanaodai nyumba zao mbili kuvunjwa (pichani), bila kulipwa fidia kwa ajili ya ujenzi wa barabara. (Picha: Abdul Mitumba, Nangaka, Mtwara.)

# Vikongwe wamwangukia Rais Samia walipwe fidia ya nyumba

**Na Abdul Mitumba, aliyekuwa Nanyumbu**



Sigele Mtehiya (90)



Laisa Mmole (97)

WAKAZI wa Kijiji cha Namasogo Kata ya Chipuputa Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara, wamemuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwasaidia walipwe fidia kufuatia nyumba zao kubolewa kupisha ujenzi wa barabara ya Mangaka -Mtambaswala.

Wakazi hao wamesema ulipaji fidia ulianza tangu mwaka jana, lakini walirukwa licha ya kwamba nyumba zao zipo ndani ya mita 22 eneo la hifadhi ya barabara hiyo inayounganisha Tanzania na Msumbiji kupitia Daraja la Umoja.

Baadhi ya wakazi hao ni vikongwe Sigele Mtehiya (90) na mumewe, Laisa Mmole (97) ambao wanadai nyumba zao ikiwemo waliyokuwa wakiishi, moja ilibomolewa nusu na nyingine iliyokuwa na mashine ya kusaga nafaka, ilivunjwa yote.

Akizungumza kwa niaba ya mumewe ambaye amepoteza uwezo wa kuongea, Sigele alisema wenzao waliokuwa wamepakana nao upande wa kushoto na kulia ukiwemo Msikiti, walilipwa, lakini wao bado.

"Mheshimiwa Rais Samia, shida ilianza wakati wa kufanyiwa uthamini wa nyumba na miti ya matunda, ambapo vijana wako kwa makusudi, waliziruka nyumba zangu. Sasa alama ya ukomo wa barabara ipo katikati ya nyumba yangu, lakini nimerukwa. Naomba unisaidie nilipwe kabla sijafa," alisema.

Alisema tangu barabara hiyo izinduliwe miaka saba iliyopita, mwanawe Stambuli Mmole, amekuwa akifuatilia katika ngazi mbalimbali za serikali, lakini huambulia vitisho na kejeli kutoka kwa baadhi ya viongozi, kwamba anapoteza muda tu na kwamba hatapata kitu cha maana.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Namasogo, Jafari Machomela, alithibitisha kuwepo kwa malalamiko kutoka kwa vikongwe hao.

Hata hivyo, na yeye pia alisema bado hajaliwa fidia ya miembe yake mitatu.

"Angalau sisi wengine tumelipwa nyumba zetu bado miembe, lakini hawa wazee kesi yao ni kubwa, maana hata wakati wa kufanyiwa uthamini wa nyumba, walirukwa licha ya kwamba zilikuwa ndani ya mita 22 za sheria ya fidia," alisema.

Mkazi mwingine wa kijiji hicho, Eleza Omar, alisema nyumba yake ilithaminiwa, lakini hadi sasa hajalipwa, hivyo kuongeza hofu kwamba zoezi hilo halijaratibiwa vizuri.

"Fidia yenyewe kama vile inatolewa kwa upendeleo, maana wengine wamelipwa, lakini mimi sijapata hadi leo," alisema Eleza na kuongeza: "Namuomba Rais Samia amtume Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aingilie kati jambo hili ili tulipwe haki zetu."

Mbunge wa Jimbo la Nanyumba, Yahya Mhata, alipoulizwa juu ya kuwepo kwa malalamiko hayo, alisema hakuwepo jimboni na kumuelekeza Mwandishi wa habari hii, awasiliane na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, ambayo alidai ndiko uratibu wa zoezi zima la kwalipa watu fidia linafanyika.

"Mwandishi nakushauri wasailiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu inayofanya uratibu wa kila siku wa jambo hilo," alisema Mhata kwa njia ya simu.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Nanyumbu (DAS), Salum Palango, alipoulizwa kama anafahamu kuwepo kwa malalamiko ya vikongwe, alisema: "Nakushauri wasiliana na Ofisi ya Wakala wa Barabara (Tanroads) Mkoa wa Mtwara ambako naye alidai ndiko kuna majibu sahihi na ya kisheria.

Mwelekeo lilipowasilana na Meneja wa Tanroads Mkoa wa Mtwara, Mhandisi Dotto John, alijibu kwa mkato tu kwamba mradi wa ujenzi wa barabara hiyo niwa kitaifa, hivyo siyo vibaya wakaulizwa viongozi wa ngazi ya kitaifa.

Hata hivyo, Mei 2, mwaka jana, mtoto wa vikongwe hao, Stambuli, alimwandikia barua ya madai ya malipo ya nyumba hizo Meneja wa Tanroads.

Barua hiyo ilipitia Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji na baada ya kuisainiwa na kugongwa muhuri, ilifikishwa kwa Katibu Tawala Wilaya ya Nanyumbu.

Kwa mujibu wa barua hiyo, ofisi ya Mkuu wa Wilaya iliipokelea Mei 9, 2022 na DAS akasaini Mei 12, 2022 na kufikishwa kwa Meneja wa Tanroads.

Katika barua hiyo, Stambuli alimuuliza Meneja wa Tanroads Mtwara kwamba, kwa nini tangu ujenzi wa barabara hiyo ukamilike mwaka 2016 na watu kuanza kulipwa, nyumba yao haijalipwa licha ya kwamba ilijengwa mwaka 1998 na ipo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara?

Meneja wa Tanroads Mkoa wa Mtwara, Mhandisi Dotto John, alijibu kwa barua ya Mei 18, 2022 yenye kumbukumbu Na.AG.190/289/01/144 ambapo alikiri kwamba amepokea barua ya malalamiko ya fidia na kujibu:-

"Tunapenda kukuarifu kwamba serikali haijaanza kulipa fidia kwenye maeneo hayo, ila itakapokuwa tayari kulipa, utaarifiwa."

Hata hivyo, sehemu ya barua hiyo ilisema 'kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na.13 ya mwaka 2007, eneo la hifadhi ya barabara ni mita 60, hivyo basi serikali ilitambua mali zote zilizomo ndani ya hifadhi ya barabara kwa kuziwekea alama ya kijani.

Kwa mujibu wa vipimo vya Tanroads, nyumba za vikongwe hao zimo mita 22.5 yaani ndani ya mita 60 zinazosemwa na kusisitizwa kwenye Sheria ya Barabara.

Kufuatia majibu hayo, Stambuli alisema yeye na wazazi wake, waliamini wakati ukifika wa serikali kulipa, nao watalipwa.

Hata hivyo, alisema licha ya kuanza kwa zoezi hlo, lakini wao bado hawajafikiwa.

Baada ya zoezi la ulipaji fidia kuanza, vikongwe hao kupitia kwa Stambuli, walimwandikia tena Meneja wa Tanroads Mtwara kwa barua ya Juni 8, 2022 ambayo ilipokelewa wilayani Juni 13 na DAS aliisaini Juni 14, 2022 na kufikishwa kwa Meneja, ikihoji kwa nini hawamo katika ulipwaji wa fidia.

Hata hivyo, majibu ya barua hiyo hayajarudi hadi sasa, badala yake Ofisi ya Meneja wa Tanroads Mtwara, inadai ilishajibu na kuituma kwa Stambuli kupitia Masjala ya Mkuu wa Wilaya, lakini na hadi sasa haijulikani ilipo.

Stambuli alisema anaambiwa tu kwamba kilichojibiwa kwenye barua hiyo ni kwamba nyumba hizo hazina sifa ya kulipwa, bila kueleza kwa nini hasa ikizingatiwa wamiliki wa nyumba zilizokuwa zikipakana na za wazazi wake, walishalipwa.

# Neema yawashukia vijana 22,000

**Na Mwandishi Wetu**

NEEMA ya ufadhili wa masomo, imewaangukia vijana zaidi ya 22,000 waliohitimu elimu ya msingi na waliofeli kidato cha nne ambao watagharimiwa na serikali kwa asilimia 100 kusomea ufundi stadi wa aina mbalimbali.

Fani zinazofadhiliwa ni ubunifu wa mitindo na ushonaji, ufundi bomba, uashi, useremala, uchomeleaji na uungaji vyuma, uchoraji na maandishi ya alama, utengenezaji wa vipuri vya mitambo, kuongoza watalii, ufundi magari na mitambo, Tehema, umeme wa majumbani, viwandani na magari, kuongoza watalii na huduma za hoteli.

Taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, ilieleza kuwa ufadhili huo ni ruzuku ambayo walengwa hawatarudisha kama inavyofanyika kwa wanaojiunga vyuo elimu ya juu nchini.

Akizungumza na MWELEKEO juzi Jumatatu, Waziri wa wizara hiyo, Profesa Joyce Ndalichako, alisema nia ya kufanya hivyo ni kuwezesha vijana kupata ujuzi mahsusi ili washindane kwenye soko la ajira na kujiajiri.

"Tunatoa ufadhili kwa vijana si chini ya 22,000 wakiwamo wenye ulemavu," alisema.

Alisema mbali ya serikali kufadhili mafunzo hayo kwa asilimia 100, wadau na washirika mbalimbali wamekuwa wakiunga mkono juhudi hizo na kugharimia vijana katika maeneo mahsusi.

Tangazo la Katibu Mkuu wa wizara hiyo lililotolewa wiki iliyopita iliyopita lilieleza kuwa, wizara hiyo imeingia mkataba na vyuo 28 ili kutoa mafunzo hayo kwa vijana.

Tangazo lilitaja sifa za watakaofadhiliwa ni vijana wa Kitanzania wenye umri wa miaka 15 hadi 35; wenye elimu ya darasa la saba na kuendelea.

Lilieleza kuwa mafunzo hayo yatatolewa na vyuo vya ufundi vya serikali pamoja na vya binafsi vilivyoidhinishwa.

"Vijana wa kike na wenye ulemavu, wanasisitizwa kuomba fursa hizi na watapewa kipaumbele katika nafasi za mafunzo haya," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

> **Vijana wa kike na wenye ulemavu, wanasisitizwa kuomba fursa hizi na watapewa kipaumbele katika nafasi za mafunzo haya..**

Naye Mkurugenzi wa Ajira na Ukuzaji Ujuzi wa Wizara hiyo, Ally Msaki, aliliambia MWELEKEO kwamba katika awamu ya kwanza ya ufadhili huo, wanategemea kupata zaidi ya wanafunzi 4,000.

"Kwa awamu ya Machi tunategemea kupata vijana 4,215 ambao watapata mafunzo ya ujuzi katika fani mbalimbali kama ilivyoelekeza taarifa yetu," alisema.

**WENYE ULEMAVU 411 WAMEANZA MASOMO**

Msaki alisema ufadhili uliotangazwa sasa ni nje ya wanafunzi 411 wenye ulemavu ambao tayari wameanza mafunzo kwenye vyuo mbalimbali nchini mwaka huu.

Mwezi uliopita, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ilitangaza ufadhili kwa wanafunzi 4,000 katika mradi wa kikanda wa 'Ajira na Ujuzi kwa Maendeleo ya Afrika (E4D)'.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kuhusu mradi huo, Ofisa Habari katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Ibrahim Ibrahim, alisema ufadhili huo unatolewa kwa vijana wasio na ujuzi wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 35.

Alisema vigezo vya ufadhili ni umri pekee kwa kuwa mradi umelenga kuwapa ujuzi vijana ili kuzalisha ajira.

"Gharama za kuendesha mafunzo zitalipwa na mradi kwa ajili ya mwombaji atakayechaguliwa kujiunga na mafunzo," alisema.

Aidha, vigezo vingine kwa mujibu wa taarifa ya serikali ni kijana wa Kitanzania, idhini ya mzazi kwa waombaji walio chini ya miaka 18 na awe na uwezo wa kufika katika vyuo vya VETA vinatekeleza mradi huo wakati wote wa mafunzo.

"Vijana wa kike na kiume wote wana fursa sawa kujiunga na mafunzo haya. Vijana wa kike wanahamasishwa kuomba," alisema.

Kozi zinazofadhiliwa katika mradi huo ni fani za uchomeleaji vyuma viwandani, ufundi bomba wa viwandani na majumbani na Mekatroniki.

Aidha, alisema lengo la programu ya E4D ni kukuza ajira katika miradi ya uwekezaji inayohitaji nguvukazi kubwa na pia kuwawezesha vijana kujiajiri.

Hata hivyo, takwimu za vijana ambao wameomba mafunzo hayo hazijapatikana kwa maelezo kuwa bado zinachambuliwa.

Mradi wa E4D umekuja wakati ambao Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwa imeanza ujenzi wa vyuo vya ufundi katika kila Wilaya.

Serikali imeazimia kujenga vyuo vya VETA ili kutoa elimu ya ujuzi maalum kwa vijana katika maeneo mbalimbali ikiwemo utaalam wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ufundi vipuri, umeme, makenika, uchomeleaji, ufundi bomba viwandani na majumbani.

Katika mwaka huu wa fedha 2022/2023, serikali imetenga Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika wilaya 62, ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo vya ufundi stadi.

Katika hatua nyingine, vijana 190 wamepata ufadhili wa asilimia 100 kupata mafunzo kwenye fani za ufundi umeme wa viwandani, vipuri, majokofu na viyoyozi, nishati ya jua na utayarishaji wa chakula.

Taarifa ya Ofisa Uhusiano wa VETA, Dora Tesha, kwa gazeti hili ilieleza kuwa vijana hao wamefadhiliwa chini ya mradi wa kukuza ujuzi majadiliano ya kijamii na ajira zenye staha kwa vijana unaofadhiliwa na Shirikisho la Wafanyakazi Denmark (DI) kwa kushirikiana na Shirikisho la Viwanda la nchi hiyo na kuratibiwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Taarifa hiyo ilieleza kuwa tayari vijana hao wamesharipoti kwenye vyuo vya VETA vya Mikumi, Dar es Salaam na Kihonda.

Katika awamu ya sasa ya ufadhili, vyuo vilivyoingia makubaliano ya kutoa mafunzo hayo ni vya maendeleo ya jamii na vya binafsi kutoka mikoa ya Dar es Salaam (1), Pwani (1), Morogoro (1), Ruvuma (2), Iringa (1), Kagera (2), Mwanza (2), Mara (2), Singida (1), Shinyanga (2), Mbeya (3), Arusha (1), Manyara (1), Geita (1), Mtwara (2), Kilimanjaro (1), Kigoma (1), Dodoma (2) na Tabora (1).



# 'Daladala wakikupandishia nauli, piga 0800110019'

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), imewataka wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wasifumbie macho upandishaji kinyemela wa nauli za daladala.

Mamlaka hiyo imesema wananchi wanaoathiriwa na vitendo hivyo, wanapaswa kutoa taarifa kwa wakaguzi wa LATRA ili hatua zichukuliwe dhidi yao. Kauli hiyo ilitolewa Ijumaa iliyopita na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano cha mamlaka hiyo, Salum Pazi, alipokuwa akizungumza na Mwelekeo kwa njia ya simu.

"Tunaomba sana wananchi watumie namba zetu 0800110019 kutoa taarifa pale wanapoona nauli za daladala zinapandishwa bila utaratibu, mara moja tutawatuma wakaguzi wetu kwenda katika eneo la tukio na kuwachukulia wahusika hatua," alisema Pazi.

Kauli hiyo imekuja wiki moja baada ya gazeti hili, kuripoti habari kuhusu kuongezwa kinyemela kwa nauli za daladala katika baadhi ya njia hasa za pembezoni mwa Jiji kwenda Gerezani Kariakoo. Uchunguzi wa Mwelekeo kuhusu kadhia hiyo, umebaini kuwa nauli za daladala zimepanda kwa karibu mara mbili ya nauli ya kawaida.

Baadhi ya njia ambazo mabasi yake yamepandisha nauli hizo ni za Tegeta Nyuki-Kariakoo, Mbagala-Kariakoo, Kisemvule-Kariakoo, Toangoma-Kariakoo, Kisewe-Kariakoo na Gongo la Mboto-Kariakoo.

Nauli halali katika njia hizo kwa safari, ilikuwa haizidi Sh. 850, lakini sasa imefikia Sh 1,300 kwa ama kwenda au kurudi Kariakoo.

Hata hivyo, hakuna mabadiliko ya viwango vya nauli yaliyofanyika kwenye tiketi za abiria na hata maandishi kuhusu nauli yaliyoko karibuni na milango ya mabasi, yanayohalalisha nauli. Hali hiyo anaashiria kuwa upandaji wa nauli hizo unafanywa kinyemela na bila ridhaa ya mamlaka iliyopewa jukumu la kusimamia usafiri wa ardhini. Uchunguzi umebaini kuwa nauli hizo zinatozwa zaidi nyakati za asubuhi na jioni ambapo wafanyakazi wa daladala, wamekuwa wakitengeneza mazingira yanayosababisha uchache wa mabasi na kuwalazimisha abiria kulipa nauli mara mbili.

Kwa mfano, mabasi yanayotoka Kisemvule, Mbagala, Kigamboni au Kisewe zinapofika nyakati hizo, yanakatisha njia katika eneo la Kamata na hivyo kuwalazimisha abiria waliopaswa kuyapanda wakiwa katika Kituo Kikuu cha Gerezani, kuyafuata na hatimaye kulipa Sh 1,300 ili wageuke nayo.

Uchunguzi wetu umebaini kuwa ukiukwaji wa kanuni hizi za usafirishaji, ulianza kidogo kidogo mwishoni mwa mwezi uliopita na sasa umekithiri na hivyo kuibua malalamiko kutoka kwa wananchi wanaotegemea usafiri wa daladala kwenda na kurudi kwenye shughuli zao za kila siku.

Kero hiyo imekuja huku kukiwa na malalamiko ya watu kuhusu kupanda kwa bei ya bidhaa na hasa za vyakula mbalimbali, jambo linalosababisha maisha kwao kuwa magumu zaidi.

Baadhi ya watu waliozungumza na gazeti hili, wamezitaka mamlaka zinazohusika kuchukua hatua dhidi ya wenye daladala zinazokiuka taratibu na hivyo kuwasababishia wananchi maisha magumu.

"Tunashangaa nauli za daladala zinapanda kiholela na hakuna maelezo yanayotolewa na mamlaka za serikali kuhusu kero hii...Ongezeko la Sh. 450 kwa safari ya Sh. 870 kutoka Kisemvule-Gerezani, Kigamboni au Kisewe si hela ndogo hata kidogo. Tunataka wahusika watueleze kwa nini inakuwa hivi," alisema Jeramiah Ludidi. Ludidi alisema kupanda kinyemela kwa nauli hizo, ni kuwabebesha wananchi mzigo mkubwa zaidi katika maisha yao ya kila siku na kwamba ni vema serikali ikachukuwa hatua za haraka kukomesha kero hiyo.

# Dk. Mpango: Tanzania salama kwa uwekezaji



Makamu wa Rais, Dk. Philipo Mpango

**Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philipo Mpango, amewataka wafanyabiashara wa kigeni kuja na kuwekeza rasilimali zao nchini, kwa kuzingatia kuwepo kwa mazingira mazuri na salama kwa uwekezaji.

Dk. Mpango alitoa wito huo katikati ya wiki iliyopita alipokuwa akifungua Jukwaa la Wafanyabiashara wa Nchi za Umoja wa Ulaya na Tanzania, lililofanyika jijini Dar es Salaam. Alisema Serikali ya Tanzania kwa kiasi kikubwa, imejitahidi kuboresha sekta za uwekezaji ili pamoja na mambo mengine, kujenga mazingira mazuri na salama kwa watu wanaotaka kuja kuwekeza rasilimali zao.

Makamu wa Rais alisema maboresho hayo ni pamoja na kurekebisha mifumo ya kodi na kuondoa urasimu uliokuwepo katika utoaji wa vibali vya maeneo ya uwekezaji na nyanja nyingine za kibiashara.

Hali kadhalika, kuimarisha sera na uwazi katika mifumo ya kibiashara ili kuongeza kasi katika uwekezaji.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, kabla ya marekebisho hayo, kulikuwa na tatizo la mifumo ya kodi na urasimu wa kupata vibali vya uwekezaji na hivyo kusababisha kero kwa watu waliokuwa na dhamira ya kuja kuwekeza.

"Huko nyuma, sheria ya kodi katika uwekezaji ilisababisha migongano katika ulipaji wa kodi hasa kwa wawekezaji. Watu walitozwa kodi mara mbili, lakini sasa sheria hiyo imefanyiwa marekebisho na hakuna tena migongano. Lakini pia utatuzi wa migogoro katika uwekezaji sasa unafanywa kwa ama kizingatia sheria zetu au za kimataifa," alisema Makamu wa Rais.

> **Nitoe wito kwa wafanyabiashara wa Tanzania, tumieni fursa hii kubadilishana uzoefu na wenzenu wa nje, tafuteni fursa huko...**

Alisema kwa misingi hiyo, Tanzania ni eneo salama mno kwa uwekezaji si tu kwa sababu za kijiografia, lakini pia jitihada zinazofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kuhakikisha kuwa taifa linapiga hatua kubwa kiuchumi.

"Kuna mazingira mazuri na salama ya kisiasa na utawala bora, haya (mazingira) yanawafanya wawekezaji wetu kutuamini na hatimaye kuwekeza rasilimali zao hapa nchini kwa manufaa yao na ya taifa letu pia," alisema Makamu wa Rais.

Dk. Mpango alitaja hatua nyingine zilizofanywa na serikali za kuwavutia wawekezaji kuwa ni pamoja na kupunguza urasimu na kuboresha utendaji wa Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania Bara na wa Kituo cha Uwekezaji cha Zanzibar.

Hatua nyingine ni za kuboresha Bandari za Mtwara, Dar es Salaam na Tanga ili kurahisisha usafirishaji wa shehena za mizigo kutoka ndani na nje na hivyo kuharakisha shughuli za kiuchumi, zikiwemo biashara.

Makamu wa Rais alisema kwa kuzingatia hayo, kuna kila sababu kwa wawekezaji wa kigeni wakiwemo wa Nchi za Umoja wa Ulaya, kuja na kuwekeza rasilimali zao katika maeneo mbalimbali.

Aliyataja maeneo ya kipaumbele na ambayo serikali inayona kuwa ni ya muhimu mno katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi kuwa ni pamoja na kilimo, viwanda vya dawa, viwanda vya ngozi, usafirishaji, utalii, nishati, madini na teknolojia ya mawasiliano.

Alisema sekta hizo ni za kipaumbele katika uwekezaji na kwamba litakuwa jambo jema kama wawekezaji wa kigeni watajitokeza na kuwekeza mitaji yao. Makamu wa Rais pia aliwataka wafanyabiashara wa Tanzania, kutumia fursa ya kushiriki katika Jukwaa hilo la kimataifa kubadilishana uzoefu na kutafuta fursa za kibiashara kutoka kwa wenzao. "Nitoe wito kwa wafanyabiashara wa Tanzania, tumieni fursa hii kubadilishana uzoefu na wenzenu wa nje, tafuteni fursa huko," alisema Makamu wa Rais ambaye pia aliushukuru Umoja wa Ulaya kwa ushirikiano wake mzuri na Serikali ya Tanzania.

# Majaliwa apiga `stop' wageni Ruangwa kubeba mizigo

**Na Abdul Mitumba, RUANGWA**

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Tanzania, Kassim Majaliwa, amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, kuwaondoa haraka vijana kutoka nje ya Ruangwa wanaofanya kazi kwenye maghala makubwa ya mazao ili nafasi zao zichukuliwe na wenyeji.

Majaliwa ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, alitoa agizo hilo kufuatia malalamiko kutoka kwa vijana wa wilaya hiyo kwamba, wanakosa ajira za kubeba mizigo ya mazao ya ufuta na korosho kwenye maghala hayo ambazo zimechukuliwa na vijana 'wageni'.

"Kuanzia sasa, Mkurugenzi wale watu wanaofanya kazi za kubeba mizigo katika maghala yetu kutoka nje ya Ruangwa, wawapishe vijana wetu wapo na wana nguvu na uwezo wa kubeba mizigo yote," alisema Majaliwa huku akishangiliwa na mamia ya watu waliokuwa wakimsikiliza.

Akisisitiza hilo, aliitaka Ofisi ya Mkurugenzi kubadilisha utaratibu wa kutumia vijana wageni kufanya kazi hiyo na kuwapa nafasi wenyeji ili waimarishe uwezo wao kiuchumi na hatimaye washiriki katika kujenga familia zao.

Alisema ghala linapokea na kuhifadhi mazao kama ufuta, korosho, kunde na mbaazi, hivyo akasema siyo haki kuweka vikundi vya watu kutoka nje ya Ruangwa kwa ajili ya kubeba mizigo wakati vikundi kama Congo, Tairi Tatu na Wandolwa, vipo na vijana wake wanamudu kufanya kazi hiyo.

Kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na gazeti hili, umebaini kuwa wakati maghala hayo yanaanza kazi miaka miwili iliyopita, waliletwa vijana kutoka wilaya mbalimbali hasa za Mkoa wa Mtwara na Ruvuma na kufanya kazi ya kushusha na kupakia mizigo kwenye magari.

Uchunguzi huo uonyesha kuwa, lengo lilikuwa vijana hao wawafundishe vijana wa Ruangwa jinsi ya kutekeleza kazi hiyo, lakini hata baada ya ujuzi huo kuwaingia wenyeji, wameendelea kung'ang'ania, hivyo kuibua malalamiko ya sasa.

Taarifa zaidi za uchunguzi zinasema, uwepo wa vijana hao kutoka nje ya Ruangwa ghalani hapo, unakingiwa kifua na baadhi ya maafisa wa halmashauri, jambo ambalo Waziri Mkuu Majaliwa alisema hataki kusikia likiendelea.

Hata hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Joseph Chonya, hakuwa tayari kuzungumzia jambo hilo licha ya kwamba wakati agizo linatolewa alikuwepo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipeana mkono na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, muda mfupi baada ya kufungua mafunzo ya Kamati ya Uongozi na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge katika Ukumbi wa Ofisi Ndogo ya Bunge, Tunguu, Kusini Unguja, Zanzibar jana. (Picha: Ofisi ya Waziri Mkuu).

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO



### Baadhi ya wanawake kutonyonesha watoto

**Machi unatambulika kama mwezi wa wanawake, ni kipindi ambacho tunawatukuza wanawake wanaotumika na kutumia uwezo wao wote kuleta matokeo chanya kwenye familia, jamii, nchi na dunia. Kero yangu ni kwa wanawake wasiopenda kunyonyesha watoto. Tunajua mnafanya mengi mazuri kulea familia lakini hili la siku hizi kwa baadhi yenu kutopenda kunyonyesha watoto ni kero kubwa na mnasababisha tuwe na kizazi kisichokuwa na afya bora. Siyo vibaya mnaposherekea mwezi wenu, mkajikumbusha wajibu huu muhimu kwa vizazi.**




## MAONI YA MHARIRI

## Samia, `umeupiga mwingi' vijana washindwe wenyewe

KATIKA ukurasa wa mbele wa gazeti hili toleo la leo, kuna habari kubwa yenye kichwa cha habari `Neema yawaangukia vijana 22,000, ni waliokwama kuingia `form one.'

Habari hii ambayo imeendelea ukurasa wa nne wa gazeti hili, inaeleza kuwa neema ya ufadhili wa masomo, imewaangukia vijana zaidi ya 22,000 waliohitimu elimu ya msingi na waliofeli kidato cha nne ambao watagharimiwa na serikali kwa asilimia 100 kusomea ufundi stadi wa aina mbalimbali. Kwa mujibu habari hiyo, fani zinazofadhiliwa kwa vijana hao ni ubunifu wa mitindo na ushonaji, ufundi bomba, uashi, useremala, uchomeleaji na uungaji vyuma. Fani nyingine ni uchoraji na maandishi ya alama, utengenezaji wa vipuri vya mitambo, kuongoza watalii, ufundi magari na mitambo, Tehema, umeme wa majumbani, viwandani na magari, kuongoza watalii na huduma za hoteli. Taarifa ya neema hiyo, ilitolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na kufafanua kuwa ufadhili huo ni ruzuku ambayo walengwa hawatarudisha kama inavyofanyika kwa wanaojiunga vyuo elimu ya juu nchini.


Akizungumza na gazeti hili la Mweleko juzi Jumatatu, Waziri wa wizara hiyo, Profesa Joyce Ndalichako, alisema nia ya kufanya hivyo ni kuwezesha vijana kupata ujuzi mahsusi ili washindane kwenye soko la ajira ni kujiajiri.

Tunachukua nafasi hii, kuipongeza serikali kwa kuja na ubunifu huu mkubwa ambao hapana shaka, utakuwa ni mkombozi mkubwa kwa vijana waliokwama kuendelea na kidato cha kwanza na pia walioshindwa kuingia kidato cha tano. Tunaamini kwamba hatua hii ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, itawasaidia vijana hao baada ya kuhitimu mafunzo hayo kujiajiri ama kuajiriwa na hivyo kuyaendesha maisha yao na familia zao. Tatizo la ajira kwa vijana ni kubwa na hili ni si changamoto inayoikabili Tanzania peke yake bali ni ya Afrika na duniani kote kwa jumla. Kwa kuwa ni changamoto ya dunia, hivyo kila serikali ya nchi husika, hujipanga kuweka mikakati ya kukabiliana nayo. Tanzania kwa upande wake, mbali ya jitihada nyingine zilizofanyika na zinazoendelea kutekelezwa, imekuja na mkakati huu ambao tunaamini kwamba utakuwa endelevu kwa lengo la kuwasaidia vijana wake. Jambo la muhimu kwa vijana sasa, ni kuhakikisha kwamba wanachangamkia fursa hii na wale watakaofanikiwa kuipata, basi waitumie vema kwa kusoma kwa bidii ili wafaulu kozi watakazopangiwa au kuziomba.

Aidha, wazazi na walezi nao kwa upande wao, wanalo jukumu la kuwahimiza vijana hao kuchangamkia fursa hiyo adhimu. Tunashauri hivi kwa sababu tunatambua miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini ikiwamo ujenzi wa barabara, viwanda, kilimo na biashara kama gereji, migahawa na saluni; kwa kuyataja kwa uchache, ni maeneo ambayo yanaweza kuwaajiri vijana hawa au kujiajiri wenyewe baada ya kuhitimu. Mweleko tunaipongeza kwa dhati serikali kutokana na uamuzi huu wa kuwapa vijana hao ruzuku hiyo ambayo hawatairejesha kama ilivyo kwa wanafunzi wengine wa vyuo vya elimu ya juu ambao hupewa mikopo.

**UMGL MEDIA** Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255693257410 / 0766005061 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255713055011 / 0621350860 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** jaridalamwekeleo@gmail.com |



Na Prosper Mhadisa
JICHO LANGU
jaridamwelekeo@gmail.com

## Kasi ya ukataji miti iende sambamba na upandaji

MWALIMU mzuri ni yule anayepandikiza maarifa katika kichwa cha mwanafunzi akitegemea kuona matunda mema ya kile alichopandikiza.

Lakini mwalimu bora, huibuka baada ya mwanafunzi wake kuja kuwa mwalimu wa mwanafunzi mwingine katika maarifa yale yale aliyoyapata mwanzo.

Kwa msingi huo, kama uwezekano wa kumpata mwalimu mzuri upo, kwanini ishindikane kumpata mwalimu bora?

Maneno haya yanajidhihirisha wazi katika Sera ya Uchumi wa Viwanda hapa nchini.

Serikali ya awamu ya tano chini ya aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli, iliasisi Sera ya Viwanda. Sera hii inatekeleza na nchi nyingi na kwa hakika, zimefanikiwa kiuchumi.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, tayari imerithi sera hiyo na kazi inaendelea ikiwemo kuvilinda viwanda vilivyoachwa na mtangulizi wake, Hayati Dk. Magufuli.

Kwa msimamo huu, ni sawa na kusema Hayati Dk. Magufuli ni mwalimu mzuri wa Rais Dk. Samia katika upandikizaji wa elimu ya masuala ya uchumi wa viwanda.

Uwekezaji katika uchumi wa viwanda, hapana budi kuwepo kwa malighafi za kukidhi kuvilisha viwanda hivyo.

Mathalani, viwanda vya kutengeneza bidhaa za mbao, karatasi na samani za aina mbalimbali, malighafi za misitu ni muhimu.

Kwa bahati nzuri ni kwamba, Tanzania imejaliwa ardhi ya kutosha yenye rutuba pamoja na hali ya hewa nzuri inayosadifu kuendesha shughuli za viwanda vinayovyotumia malighafi ya misitu.

Kabla ya sera ya uchumi wa viwanda haijashika kasi, misitu ya mbao ilipatikana kwa wingi hususan katika mikoa ya Njombe na Iringa.

Hata hivyo, kwa sasa baada ya sera hii kushika kasi, misitu ya namna hiyo, imeanza kupungua kwa kasi bila kuwepo kwa juhudi za makusudi za kupanda miti kwa wingi kuchukua nafasi ya iliyokatwa.

> **Uwekezaji katika uchumi wa viwanda, hapana budi kuwepo kwa malighafi za kukidhi kuvilisha viwanda hivyo...**

Ukitembelea mikoa hiyo kwa sasa, utabaini kasi ya uvunaji wa misitu tofauti na upandaji.

Viwanda vingi vilivyopo katika mikoa hiyo, vinamilikiwa na wawekezaji wa kutoka nje ya nchi.

Wawekezaji hao wamekuwa wakivuna misitu ya mbao bila ukomo, lakini hakuna juhudi za upandaji wa mti mingine ya kuchukua nafasi ya iliyovunwa.

Hali hii kama itaachwa iendelee pasipo kuwepo kwa mwongozo, ipo hatari malighafi hiyo itaadimika siku za usoni.

Kwa msingi huo, ipo haja ya kuwepo kwa sera ya kuwabana wawekezaji wapande miti mitatu hadi minne kwa kila mti mmoja unaokatwa.

Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kulinda mazao ya misitu ili iwe endelevu.

# CCM kuendelea kuisimamia serikali bega kwa bega

**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kitaendelea kuisimamia serikali bega kwa bega ili kuhakikisha kero zinazowakabili wananchi katika nyanja zote zinapatiwa ufumbuzi kama ilani inavyoelekeza.

Aidha, kimewaomba wananchi waendelee kushirikiana na serikali yao kwa kuwa ahadi nyingi zimetekelezwa na matokeo yake yanaonekana kwenye maeneo mengi.

Akiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto, Katibu Halmashauri Kuu ya CCM (NEC), Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema, alisema utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara, madarasa, zahanati, uboreshaji wa bandari, upelekaji wa umeme vijijini na ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Tanga hadi Uganda, ni hatua ya kusogeza huduma muhimu kwa wananchi na kuwezesha ukuaji wa biashara na uchumi kwa jumla.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo ambayo inaendelea nchi nzima, ni dalili nzuri kwa chama hicho kuendelea kukubalika kwa umma na kwamba hilo halitaifanya CCM ibweteke na kuacha kuisimamia.

"Licha ya kwamba kazi kubwa imeshafanyika, bado CCM tuna kazi ya kuhakikisha tunakamilisha yale yote tuliyoahidi katika ilani yetu ya 2020/2025," alisema Mjema.

Aliongeza: "Kuhusu ajira kwa vijana Mheshimiwa Rais kwenye kilimo ametoa Sh. bilioni 900 kwa ajili ya mashamba ya umwagiliaji kuelekea uchumi wa kimkakati."

Mjema alisema amekwishaongea na Mkuu wa Mkoa wa Tanga na amemhakikishia kwamba serikali mkoani hapa imekwishatenga mashamba kwa ajili ya vijana.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anafanya jitihada kubwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora zikiwamo za afya, elimu, miundombinu na biashara.

Alisema kasi ya utekelezaji wa ilani chini ya Dk. Samia inatoa picha ya ushindi mwaka 2025 kwani mengi yametekelezwa.

Alisema CCM itaendelea kuisimamia serikali yake kwa kufuatilia utekelezaji wa ilani nchi nzima ili kuhakikisha watendaji wa serikali hawalali bali wanawahudumia wananchi ambao wamekiamini chama hicho. Kwa upande wake, mbunge wa Bumbuli (CCM), ambaye pia ni Waziri wa Nishati, Januari Makamba, alisema kwa mwaka huu wa fedha, serikali imetenga Sh. 206 Bilioni kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye vijiji vyote vya mkoa wa Tanga.

Alisema hivi sasa Mkoa wa Tanga unapokea umeme moja kwa moja kutoka gridi ya taifa na kwamba marekebisho yanayoendelea ya kuboresha upatikanaji wa umeme mkoani hapa yamefumua na kusuka upya njia za umeme jambo lililowezesha kupata nishati hiyo moja kwa moja toka Ubungo, Dar es Salaam hadi Hale.

Alisema zoezi linayofuata ni kusuka njia ya umeme toka Hale hadi Majani Mapana kazi ambayo itamaliza kabisa tatizo la umeme mkoani hapa.

Kwa upande wa mafuta, alisema kibali cha ujenzi wa bomba kutoka Tanga hadi Uganda kipo tayari na kitatolewa muda wowote kuanzia sasa. Alisema ujenzi wa bomba hilo ni hatua nzuri ya kukuza uchumi wa Tanga na nchi kwa ujumla pamoja na kuchochea biashara na kuzalisha ajira.

Alisema mradi mwingine ambao unatekelezwa na serikali mkoani hapa ni ujenzi wa bomba la gesi kutoka Dar es Salaam-Tanga hadi Mombasa, ambalo litaibua fursa nyingi za uwekezaji na biashara. Kuhusu maji, Makamba alisema serikali imeanza kutekeleza mradi mkubwa wa Mowe akieleza kuwa utakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 48 wakati mahitaji ya mkoa wa Tanga ni lita milioni 37.

Akizungumzia miundombinu, alisema bandari ya Tanga imeendelea kuboreshwa na kuongeza ufanisi hivyo imeanza kupokea meli kubwa za mizigo. Alisema serikali pia inapanua uwanja wa ndege wa Tanga na kuuunganisha mkoa huo na Dar es Salaam kwa njia ya barabara.

Alisema tayari ujenzi wa barabara ya Tanga-Pangani-Bagamoyo hadi Dar es Salaam imeanza.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba, alisema katika kipindi cha miaka miwili ya Rais Dk. Samia madarakani, mkoa wake umepokea Sh. Trilioni 1.2 za miradi ya maendeleo.

Alitaja baadhi ya miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa ni miundombinu ya barabara, bandari na madaraja.

Kwa upande wa elimu, alisema katika kipindi hicho, shule za sekondari 14 zimejengwa na kwamba wanapata maji safi kwa asilimia 90.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi walalamikia utaratibu wa upatikanaji wa mikopo inayotolewa na Halmashauri kupitia mfuko wa Wanawake, Vijana na wenye ulemavu, jambo ambalo Mjema alitaka litatuliwe kwa kuweka dawati la kuwaelimisha wananchi kwenye kila Halmashauri.

"Mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake na vijana litatuliwe," alisema.

## Kina cha maji Bwawa la Mwl. Nyerere chafikia mita 134.39

**Na Mwandishi Wetu**

KINA cha maji katika Bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP) katika Mto Rufiji, mkoani Pwani, kimeendelea kuongezeka na sasa kimefikia urefu wa mita 134.39 kutoka usawa wa bahari.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Elihuruma Ngowi, alisema utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 81.82.

Alisema kazi inaendelea kufanyika na kwamba mategemeo ni kukamilisha ujenzi kama ilivyopangwa.

"Hadi leo (jana), kina cha maji katika Bwawa la JNHPP, kimefika urefu wa mita 134.39 toka usawa wa bahari huku utekelezaji wa mradi ukiwa umefikia asilimia 81.82," alisema.

Mto Rufiji, ndiyo chanzo kikuu cha maji ya mradi huu unaotarajiwa kuzalisha megawati 2,115 za umeme utakapokamilika, lakini pia Mto Kilombero unachangia asilimia 65, Mto Luwegu asilimia 19 na Ruaha Mkuu asilimia 15.

Aidha, njia ya kuchepusha maji, ina urefu wa mita 703 na upana ni kipenyo cha mita 12.

Mradi wa JNHPP unaoshika nafasi ya kwanza kwa ukubwa kwa miradi yote inayotekelezwa katika nchi za Afrika Mashariki na ni wa nne kwa miradi yote inayotekelezwa Afrika.

Mradi unaoshika nafasi ya kwanza Afrika ni wa Grand Ethiopian Renaissance Dam (6,400 MW) uliopo nchini Ethiopia, namba mbili ni ule wa Batoka George Hydroelectric Dam (2,400 MW), wa nchini Zambia katika Mto Zambezi na wa tatu ni mradi wa Caculo Cabaco Hydroelectric Dam (2,172 Mw) wa nchini Angola.

Gharama za mradi huu wa Bwawa la Nyerere hadi utakapokamilika ni zaidi ya Sh. trilioni 6.5 na tayari mkandarasi ameshalipwa asilimia 65 ya kiasi hicho.

Fedha hizo zinametokana na makusanyo ya kodi mbalimbali na hatua hiyo imeifanya serikali isidaiwe na mkandarasi.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Desemba 22, mwaka jana, alizindua rasmi ujazaji wa maji katika bwawa hilo lenye ukubwa wa kilometa 915 za mraba.

Uzinduzi huo ulishuhudiwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Marais Wastaafu, Ali Hassan Mwinyi na Dk. Jakaya Kikwete.

Katika tukio hilo, marais hao wastaafu, walitunukiwa Tuzo Maalum kwa michango yao katika mradi huo nyakati za uongozi wao.

Viongozi wengine waliotunukiwa tuzo hizo ni Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, ambaye tuzo yake ilipokelewa na mtoto wake, Makongoro Nyerere, Hayati Benjamin Mkapa, ambaye tuzo yake ilipokelewa kwa niaba yake na Mzee Mwinyi na Joseph Magufuli, aliyepokea kwa niaba ya baba yake, Hayati Dk. John Magufuli.

Sherehe hizo zilihudhuriwa pia na Waziri wa Nishati, January Makamba, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, mawaziri na wabunge.

## Zahanati iliyojengwa miaka 15 yaanza kutoa huduma

**Na Mwandishi Wetu, Pwani**

ZAHANATI ya Kitongoji cha Pingo Kata ya Pera mkoani Pwani iliyoanza kujengwa miaka 15 iliyopita, imeanza kutoa huduma kwa wakazi wa kitongoji hicho.

Kukamilika kwa zahanati hiyo, kumeongeza chachu na upatikanaji wa vifaa tiba vilivyotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, vilivyokabidhiwa kwa halmashauri hiyo vyenye thamani ya Sh. milioni 350, kisha kusambazwa kwenye zahanati 11.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya uzinduzi na kukabidhi vifaa hivyo kwa Mwenyekiti wa Kitongoji cha Pera, Idi Fuko, Diwani wa kata hiyo, Jackson Mkango, alisema amefurahi kukamilika kwa zahanati sanjari na kupokea vifaa hivyo.

"Shukrani za kipekee kwa Rais Samia kwa msaada mkubwa anaoendelea kutupatia Kata ya Pera, Mbunge wangu Ridhiwani Kikwete pamoja na Madiwani wenzangu wote, hadi kukamilika kwa zahanati imegharimu Sh. milioni 140," alisema Mkango.

Nao wakazi wa kitongoji hicho, Mwajuma Abdallah na Shaban Juma, kwa nyakati tofauti waliishukuru serikali kwa kumalizia zahanati hiyo, iliyowaondolea adha ya kutembea umbali mrefu mpaka Chalinze kufuata huduma.

Kwa upande wake, Fuko aliwaomba wakazi wa eneo hilo, kuitumikia vizuri pamoja na kulinda miundombinu yake.

"Tunaishukuru serikali kwa kutukamilishia zahanati yetu, tunashuhudia leo (juzi), imeanza kuwapatia wakazi huduma, niwaombe Wanapingo wenzangu, tuitumie vizuri zahanati yetu ambayo imeletewa vifaa tiba vya kisasa," alisema Fuko.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Zahanati hiyo, Nuru Mhami, alisema wananchi walikata tamaa baada ya kuchelewa kukamilika kwa miaka 15, huku akiishukuru serikali kwa kuwapatia vifaa tiba vya kisasa.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu

> **Tunaishukuru serikali kwa kutukamilishia zahanati yetu, tunashuhudia leo...**

HABARI KUTOKA ZANZIBAR



# ACT-Wazalendo yaishauri SMZ kuhusu utalii

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman (pichani), ameishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kuweka utaratibu mzuri wa uwekezaji katika maeneo yenye utalii ili wananchi wafaidike na uwekezaji katika maeneo yao.

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wanachama wa chama hicho katika mkutano wa hadhara uliofanyika Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja mwishoni mwa wiki.

Alisema Nungwi ni eneo maarufu kwa uwekezaji mwingi, lakini hakuna wanachofaidika kutokana na kutokuwa na mipango mizuri ya uwekezaji na kuwafanya watu wengi wakate tamaa.

"Sisi Zanzibar, tutakachofaidika nacho ni kilichopo Zanzibar", alisema.

Alifafanua kwamba wananchi walitegemea kama kuna mtu kaja kuwekeza Nungwi na kufanya biashara, basi wananchi nao wafaidike.

Alisema iwapo kungelikuwa



na utaratibu mzuri, watu wa Nungwi wangefurahia uwekezaji huo. Aliongeza kuwa kutokana na kutokuwa na utaratibu mzuri,mtu anaweza kuja Zanzibar na kukodi ardhi akafanya biashara, akapata faida na baadaye akaondoka.

Naye Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Juma Duni Haji, alisema wananchi wa Zanzibar lazima wawe na imani na chama hicho sambamba na ahadi zinazotolewa na kwamba ACT ndicho chama chenye uwezo na dira ya kuifikisha Zanzibar

> **Sisi Zanzibar, tutakachofaidika nacho ni kilichopo Zanzibar**

kwenye maendeleo. Hivyo aliwataka wananchi washirikiane kwa kujenga umoja na maridhiano kwa kuwa chama chake kinaamini na kuhubiri sera hiyo bila ya viongozi wake kuchoka kwa muda mrefu sasa.

Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, aliwaambia wananchi wa Zanzibar kuwa nchi yao ni nzuri sana na inaongozwa kwa kiwango kikubwa na uchumi wake unategemea kwa Bandari na Uwanja wa Ndege.

Alifafanua kuwa maeneo hayo ni muhimu kwa sababu theluthi mbili ya uchumi wa Zanzibar, unategemea biashara na utalii.

# Mwanaharakati atoa kauli nzito dhidi ya kampuni za vileo Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAHARAKATI wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ali Makame Issa, ameshauri kampuni za vileo zinazojihusisha na biashara za magendo zifutwe ili kulinda upotevu wa mapato ya serikali.

Mwanaharakati huyo aliyasemwa hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa Jumuiya ya Watu wasiona Zanzibar baada ya kampuni moja ya visiwani humu, kutuhumiwa kuingiza vileo vya magendo Febuari 12, mwaka huu.

"Biashara ya magendo inasababisha hasara kubwa ya mapato kwa serikali hasa magendo ya vileo kutokana na thamani yake, mamlaka za ukusanyaji kodi lazima zichukue hatua kudhibiti mianya hiyo," alisema Makame.

Akifafanua sakata hilo, alisema kampuni zilizopewa kibali cha kuingiza pombe Zanzibar ni tatu.

Alizitaja kampuni hizo kuwa ni Scoch, One Stop Center na ZMMI ambazo ndizo zilizoshinda zabuni kwa mujibu wa sheria ya vileo ya mwaka 2020.

"Sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi inazungumza kampuni mwisho tatu za kuingiza vileo Zanzibar," alisema.

Kwa mujibu wa Mwanaharakati huyo, lengo la kutungwa kwa Sheria ya Vileo ya mwaka 2020, ni kuziba mianya ya ukwepaji wa kodi kupitia biashara ya vileo pamoja na uingizaji holela wa pombe Zanzibar.

Hata hivyo, iliipongeza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), kwa kuahidi kuchunguza sakata hilo muda mfupi baada ya kujitokeza.

"Nichukue nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi wa ZAECA kwa hatua anazochukua katika kukabiliana na vitendo vya kuhujumu uchumi ikiwemo biashara za magendo," alisema.

Aidha, alisema inasikitisha kuona Bodi ya Vileo imelegeza masharti kwa kushindwa kusimamia sheria ipasavyo, jambo ambalo linatia wasiwasi wa kuwepo kwa mianya ya rushwa ndiyo maana Sheria ya Vileo inashindwa kusimamiwa ipasavyo. Hata hivyo, alimpongeza Rais wa Zanzibar kwa hatua anazoendelea kuchukua za kupambana na ubadhirifu wa mali za umma tangu kushika madaraka mwaka 2020.

Alisema misingi ya utawala bora inaonekana kuimarika Zanzibar kutokana na kuongezeka kwa uwajibikaji kwa watumishi wa umma na serikali kufanikiwa kudhibiti vitendo vya ubadhirifu wa mali za umma pamoja na mafisadi kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Akizungumzia suala hilo, Msimamizi wa kampuni ya MGW 2014 Enterprises, Ali Seif, alikanusha kampuni yake kuhusishwa na biashara ya magendo.

"Kuna vita vya kibiashara vinaendelea na wafanyabiashara wakubwa hawapendi kuona wafanyabiashara wadogo wakinyanyuka, sisi vileo tunavyosambaza tunanunua kutoka katika kampuni zilizopewa vibali vya kuingiza vileo Zanzibar," alisema Seif wakati akizungumza na waandishi wa habari.

# Wafurahishwa huduma nzuri za Kituo cha Afya

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

WAKAZI wa Kijiji Cha Unguja Ukuu visiwani humu, wamefurahia juu ya upatikanaji wa huduma za afya zinazotolewa na madaktari wanaofanya kazi katika Kituo cha Afya Unguja Ukuu.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi juzi, baadhi ya wakazi waliokutwa wakipatiwa huduma katika kituo hicho, walisema madaktari wapo vizuri na wanashukuru kwa ukarimu wao wanaouonesha kwa muda wote.

Amina Ali, mkazi wa Unguja Ukuu Kae Bona, alisema tofauti na watu wengi wanavyowafikiria wahudumu wa afya, lakini katika kituo chao wamekuwa wawakihudumia vizuri.

"Tunafurahia sana kwani madaktari pamoja na wahudumu wote, wamekuwa wakitoa huduma nzuri na kutupa maneno mazuri kila tunapokuja kupatiwa huduma," alisema.

Hata hivyo, alisema imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya watu kuwalalamikia madaktari au wahudumu wa afya, lakini katika kituo chao, jambo hilo halipo.

"Daktari au mhudumu wa afya, ni binadamu wakati mwingine huteleza kama anavyoteleza mtu mwingine, kwa hivyo inapotokea hilo, kwetu sisi huchukulia ni bahati mbaya hasa kwa kuwa hawana utamaduni huo," alisema.

Aidha, alisema jamii inayozunguka kituo hicho, imekuwa na ushirikiano wa hali ya juu kuhakikisha kituo hicho kinakuwa bora.

Mmoja wa madaktari kituoni hapo, Jabir Zahim Khamis, alisema kituo chao hutoa huduma zote sawa na zitolewazo na vituo vya afya na zinapatikana kwa wakati,

Alizitaja huduma hizo kuwa ni za wagonjwa wa nje zinazojumuisha maabara, dawa, kumuona na daktari, meno, uzalishaji, huduma za mama na watoto na chanjo.



Leo yetu ndiyo kesho yetu

Mwelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

Jumatano Februari, 22-28, 2023




Jarida hili haliuzwi



# Bwawa la Nyerere zaidi ya mradi

UK. 12 & 13



UK. 11

## Samia aweka historia ujenzi wa madarasa

## Uza sana kuliko kununua

UK. 16



Elimu



# Samia aweka historia ujenzi wa madarasa

## Kila siku madarasa 80, kwa saa matatu !

**Na Mwandishi Wetu**

NI historia. Ndiyo lugha sahihi inayofaa kutumika baada ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dk. Samia Suluhu Hassan, kufanya miujiza kwa kufanikiwa kujenga madarasa 8,000 ya sekondari nchi nzima kwa siku 100 tu.

Aidha, ujenzi wa madarasa hayo, ulienda sambamba na samani zake kwa kila darasa.

Hayo yalisemwa na Rais Dk. Samia hivi karibuni kupitia katika taarifa yake fupi kwenye mtandao wa 'Twitter.',

Rais Samia alisema katika siku 100, serikali yake ilifanikiwa kujenga madarasa ya sekondari 8,000.

Alisema kwa msingi huo, hakuna mwanafunzi atakayekosa nafasi ya kusoma kutokana na changamoto ya ukosefu wa madarasa.

"Katika siku 100 zilizopita, serikali imefanikiwa kujenga madarasa ya sekondari 8,000 pamoja na samani zake nchi nzima ambayo yataanza kutumika wiki ijayo," alisisitiza Rais Dk. Samia na kuongeza:

Kwa hesabu, hii inamaanisha kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita ilikuwa ikijenga madarasa 80 kila siku nchini nzima.

Aidha, inaonyesha kuwa kwa takwimu hizo, kila saa chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia, yalijengwa madarasa matatu nchi nzima.

"Hatua hii ya kihistoria, ni ukombozi kwa wanafunzi zaidi ya 400,000."

Katika miaka ya nyuma, kulikuwepo na changamoto kubwa la uhaba wa madarasa na samani hususan kwa wanafunzi wanaoingia kidato cha kwanza na darasa la kwanza.

Hali hiyo ilisabisha wanafunzi wengi ama kukosa nafasi ya kuendelea kidato cha kwanza na wale wa kuanza darasa la kwanza, kushindwa kuanza masomo kutokana na uhaba wa madawati.

Shule za msingi na sekondari nchini, zilifunguliwa Januari 9, mwaka huu. Kwa kitendo hiki, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia, imeweka historia ambayo haijawahi kufanyika tangu nchi ipate Uhuru.

**100**

**Rais Samia alisema katika siku 100, serikali yake ilifanikiwa kujenga madarasa ya sekondari 8,000.**



**Katika siku 100 zilizopita, serikali imefanikiwa kujenga madarasa ya sekondari 8,000 pamoja na samani zake nchi nzima ambayo yataanza kutumika...**

Afya


Na Waandishi Wetu

UGONJWA wa tezi dume ni moja ya maradhi ambayo kwa sasa yamekuwa yakiwasumbua wanaume wengi hapa nchini.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), tezi dume ni tezi inayopatikana kwa jinsia ya kiume.

Tezi hii ina kazi ya kutengezeza majimaji meupe mepesi yenye unato kidogo. Majimaji haya husaidia mbegu za kiume kutembea kwa urahisi.

Tezi dume iko mwishoni mwa kibofu cha mkojo. Pia inauzunguka mrija unaounganisha kibofu cha mkojo na na mrija wa mkojo wa uume (urethra) na iko mbele kidogo ya utumbo mpana ndani ya fupa la nyonga.



# Zijue dalili za tezi dume na tiba yake

### Saratani ya tezi dume ni nini?

Saratani ya tezi dume maana yake ni tezi dume imepata ugonjwa wa saratani..Na hii hutokea pale ambapo chembechembe hai za tezi huasi na kuanza kujigawanya bila kufuata utaratibu wa mfumo wa mwili, chembechembe asi hizi mwishowe hutengeneza vivimbe hatari ndani ya tezi dume na hatimaye husambaa mwilini.

Visababishi hatarishi kwa saratani ya tezi dume
Umri mkubwa kuanzia miaka 50
Nasaba (ukoo wenye historia ya saratani)
Lishe hatarishi ikiwemo nyama nyekundu kwa wingi, mafuta/samli,maziwa ya krimu.
Unene uliokithiri
Ukosefu wa mazoezi
Upungufu wa virutubisho,mfano vitamin D.
Maambukizi ya mara kwa mara kwenye tezi dume

### DALILI

- Udhaifu katika utoaji wa mkojo, mkojo hauishi.
- Kukojoa mara kwa mara.
- Mkojo uliochanganyikana na damu.
- Kukojoa kwa shida.
- Maumivu ya kiuno na mifupa ya nyonga.
- Wagonjwa wengi huanza maumivu ya nyonga kama ni dalili za awali.
- Udhaifu katika utoaji wa mkojo pia kunaweza kutokea kwa kuvimba kwa tezi dume bila ya saratani.
- Kushindwa kumaliza mkojo ni ishara tosha ya kuwa tezi dume imeathirika.

### UCHUNGUZI

Wanaume wote wanapaswa kufanya uchunguzi wa saratani ya tezi dume kuanzia miaka 50. Kwa wale wenye historia katika familia wanapaswa kuanza wakiwa na umri wa miaka 45.

Uchunguzi unafanyika kwa njia zifuatazo:-

- Uchunguzi kwa cancer marker kwa kuchunguza damu (PSA).
- Uchunguzi kwa njia ya kipimo cha njia ya haja kubwa (DRE)
- Biopsy.
- Ultra sound.
- X-ray.
- Bone scan.

### Jinsi ya kutibu saratani ya tezi dume

- Upasuaji.
- Mionzi
- Dawa ya saratani
- Homoni.

Matibabu hutegemea

- Ngazi na ukali wa ugonjwa.
- Je, ugonjwa upo ndani ya tezi dume tu au umesambaa.
- Umri na afya ya mgonjwa.
- Magonjwa ambatanishi na saratani hiyo, shinikizo la damu, matatizo ya moyo na kisukari.

### TIBA

### UPASUAJI

- Kuondoa tezi dume yote peke yake inaweza ikatosha.
- Kuondoa tezi dume na tezi jirani.
- Kuondoa tezi dume na kuhasi
- Kuondoa tezi dume kidogo kupitia njia ya mkojo na kumpa mgonjwa tiba shufa.

> **Na hii hutokea pale ambapo chembechembe hai za tezi huasi na kuanza kujigawanya bila kufuata utaratibu wa mfumo wa mwili...**

### MIONZI

- Sawa na upasuaji inaweza kuondoa ugonjwa iwapo haujasambaa.
- Mionzi pia hutolewa kama tiba shufaa.

### DAWA YA SARATANI

Baadhi ya wagonjwa hufaidika na tiba hii, dawa hutolewa kwa muda mfupi na kufuatilia maendeleo ya mgomjwa kwa kufanya PSA,dawa inaweza kuwa moja au mchanganyiko.

### HOMONI

Hutolewa mfullulizo kwa njia ya vidonge au sindano.

### Ufuatiliaji wa karibu


Ni muhimu kufuatilia hali ya tezi isirejee baada ya ugonjwa kutibiwa kwa kufanya kipimo cha PSA mara kwa mara angalau miezi mitatu mara moja. Athari zitokanazo na matibabu mbalimbali yaliyotajwa.

### Upasuaji

Unaweza kusababisha kupoteza nguvu za kiume na kutoweza kuzuia mkojo.

Homoni

- Homoni huongeza joto mwilini
- Kupungukiwa na nguvu za kiume



Uchumi

# Bwawa la Nyerere zaidi ya mradi

## Nambari wani Afrika Mashariki, Afrika wa nne

**Na Prosper Mhadisa**



MOJA ya miradi mikubwa kuwahi kutekelezwa hapa nchini, ni mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Julius Nyerere katika Mto Rufiji mkoani Pwani.

Ni mradi unaoshika nafasi ya kwanza kwa ukubwa katika miradi yote inayotekelezwa katika nchi za Afrika Mashariki na ni wa nne kwa miradi yote inayotekelezwa Afrika.

Mradi unaoshika nafasi ya kwanza Afrika ni wa Grand Ethiopian Renaissance Dam (6,400 MW) uliopo nchini Ethiopia, namba mbili ni ule wa Batoka George Hydroelectric Dam (2,400 MW), wa nchini Zambia katika Mto Zambezi na wa tatu ni mradi wa Caculo Cabaco Hydroelectric Dam (2,172 Mw) wa nchini Angola.

Gharama za mradi hu
Nyerere hadi utakapoka
ya Sh. trilioni 6.5 na tay
ameshalipwa asilimia 65 y

Fedha hizo zinametokan
ya kodi mbalimbali na hatu
serikali isidaiwe na mkand

Rais Dk. Samia Suluhu H
22, mwaka jana, alizindua
maji katika bwawa hilo l
kilometa 915 za mraba.

Uzinduzi huo ulishuhud
mbalimbali wakiwemo Ma
Hassan Mwinyi na Dk. Jaka

Katika tukio hilo, mara
walitunukiwa Tuzo Maalu
yao katika mradi huo ny
wao. Viongozi wengine
tuzo hizo ni Baba wa
Mwalimu Julius Nyerere, a
ilipokelewa na mtoto wa
Nyerere, Hayati Benjamin
tuzo yake ilipokelewa
na Mzee Mwinyi na Jo
aliyepokea kwa niaba ya b
Dk. John Magufuli.

Sherehe hizo zilihudhur
wa Nishati, January M
wa Bunge la Jamhuri ya
Tanzania, Dk. Tulia Acks
wabunge. Pia viongozi wa
serikali na wa vyama mba
Waziri wa Mambo ya Nje
Shoukry na Waziri wa Nyu
inayojenga mradi huo, pia
uzinduzi huo.

Mto Rufiji, ndiyo chanzo
mradi huu unaotarajiwa ku
2,115 za umeme utakapoka
Mto Kilombero unachangi
Luwegu asilimia 19 na Rua
15. Aidha, njia ya kuche
urefu wa mita 703 na upan
mita 12.

Kwa mujibu wa Mkur
wa Shirika la Umeme Tan
Mhandisi Maharage Chan
kwenda juu ni mita 131.



uu wa Bwawa la
amilika ni zaidi
yari mkandarasi
a kiasi hicho.
na na makusanyo
ua hiyo imeifanya
darasi.
Hassan, Desemba
a rasmi ujazaji wa
enye ukubwa wa

diwa na viongozi
rais Wastaafu, Ali
aya Kikwete.
is hao wastaafu,
m kwa michango
akati za uongozi
waliotunukiwa
a Taifa, Hayati
ambaye tuzo yake
ake, Makongoro
a Mkapa, ambaye
kwa niaba yake
oseph Magufuli,
baba yake, Hayati

riwa pia na Waziri
Iakamba, Spika
a Muungano wa
on, mawaziri na
ngazi nyingine za
limbali vya siasa.
wa Misri, Sameh
mba wa nchi hiyo
a walikuhudhuria

kikuu cha maji ya
uzalisha megawati
amilika, lakini pia
a asilimia 65, Mto
ha Mkuu asilimia
epusha maji, ina
na ni kipenyo cha

ugenzi Mtendaji
zania (Tanesco),
de, urefu wa tuta




**Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Desemba 22, mwaka jana, alizindua rasmi ujazaji wa maji katika bwawa hilo lenye ukubwa wa kilometa 915 za mraba...**

Mhandisi Chande anasema shirika hilo lina mpango wa kuzalisha megawati 5,000 za umeme na ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere, utaongeza megawati 2,115 .


Mradi huu, pia umezalisha fursa za ajira 12,275 ambapo kati ya hao, wazawa ni 11,164 sawa na asilimia 90.97 waajiriwa kutoka nje ya nchi ni 1,111 sawa na asilimia 9.1.

Mradi huu pia utakuwa na uwezo wa kuimarisha na kufungua fursa nyingi za utalii hususan katika eneo la Kusini mwa Tanzania ndani ya Hifadhi ya Nyerere na hivyo kutoa ajira za moja kwa moja na nyinginezo ndani ya mradi. Kupitia fursa hiyo ya utalii, Taifa litanufaika kwa kupata fedha za kigeni kutoka kwa watalii wa nje ya nchi.

Kadhalika, mradi huu utaimarisha shughuli za viwanda katika uzalishaji.

Ujenzi wa mradi huu umezingatia mazingira ikiwemo kuruhusu maji kuchepuka nje ya bwawa ili kutoa nafasi kwa viumbe vingine kuendelea kuishi. Hali kadhalika shughuli nyingine za











siasa

# Nyerere: Chama ni cha dini zote, makabila yote na koo zote

**Na Mwandishi Wetu**

TANU na Raia, ni kitabu kilichoandikwa na Hayati Mwalimu Julius Nyerere, mwaka 1962 ikiwa ni mwaka mmoja tu tangu Tanganyika kupata Uhuru.

Mwalimu Nyerere katika kitabu hicho, alielezea kwa kina lengo la kuanzishwa kwa TANU. Tujikumbushe maadhui ya kitabu hicho muhimu ambayo kimsingi, ndiyo lengo la Chama Cha Mapinduzi (CCM).

TANU ilipoanzishwa na kufanikiwa kuuleta Uhuru, haikudhamiria kuwafanya wananchi wengi wa Tanganyika wawe watumwa wa viongozi wachache na wanachama wachache wa chama hicho wala uraia wa watu wengi uhodhiwe na kundi hilo la uchache na hao wachache.

Lengo la TANU ilipoanzishwa halikuwa kuwaletea Uhuru viongozi wachache na wanachama wachache wa chama hicho fursa na nguvu ya kuwafanya Watanganyika wengi wawe watumwa wa uongozi wa kundi la watu wachache kwenye Chama tawala.

Aidha, upatikanaji wa Uhuru wa Tanganyika haukuwa wa kuwawezesha viongozi wachache na wanachama wachache wa TANU kuuhodhi uraia wa watu wengi, bali ni Uhuru wa raia wote wa Watanganyika bila ubaguzi. Suala la hadhi inayotokana na Uhuru lilipojitokeza kwa vitendo kwa baadhi ya watu, katika kitabu 'TANU na Raia' alichokiandika Aprili 1962, Mwalimu Nyerere anasema Serikali ya TANU ilichukua hatua za haraka kuwaondoa mashaka waliohusika kuwa ni kwa raia wote, bila ubaguzi.

" TANU haina dini, au kabila au ukoo. TANU ni ya dini zote, na makabila yote na koo zote. Ni TANU peke yake, basi ambayo ina wajibu mkubwa kushughulika na shida za watu wa aina yo yote.

Wakati mwingine huwa tukizungumza shida za Jumuiya, yaani siyo shida za mtu mmoja mmoja," Rais Mwalimu Nyerere anajulisha.

Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba kwa kweli hizo ni shida za Jumuiya, siyo uzushi wetu wenyewe kwa faida yetu wenyewe. Mambo tunayo yazungumza katika mikutano yetu hayana budi yatokane na watu wenyewe huko Vijijini kwao.

Kanuni ninayo jaribu kueleza hapa ni kwamba Chama cha watu ni chama cha watu. Viongozi wake wanatokana na watu wale wale; shida zao ni shida za watu wale wale. Tukisahau kanuni hii hatuwezi kuwa Chama cha watu, na hatustahili kuwa chama cha watu. Ikiwa sisi ni viongozi wa watu, na Chama chetu ni cha watu, basi sisi hakuna shida yo yote ya watu ambayo twaweza kusema kuwa haituhusu,Julius K. Nyerere, Rais wa TANU anaeleza kwenye, kitabu hicho cha Aprili, 1962. Katika kuvihukumu vitendo vyetu kama ni vizuri, au ni vibaya, hatuna budi tujiulize: Je, vinasaidia au vinapinga kutimiza shabaha ya Chama chetu ?Tulipokuwa tukiondoa serikali ya kikoloni tulikuwa na shabaha pia ya kuyaondoa maovu yote yaliyoandamana na serikali ya kikoloni.

Aidha, Mwalimu Nyerere anasisitiza uwajibikaji kwa kusema "Swali ambalo hatuna budi tujiulize ni hili:


Tunamwomba kila raia kufanya kazi kwa bidii ili tuondoe umaskini wa nani? Umaskini wa viongozi wa TANU? Au wa watumishi wa serikali au wa watu wachache wenye elimu, au nguvu, au bahati au ujanja? Au shabaha yetu ni kuondoa umaskini wa kila mtu kama vile shabaha yetu ya kwanza ilikuwa ni kuleta uhuru na heshima kwa kila mtu?"

Mwalimu anatahadharisha majibu ya jumla ya viongozi, wanachama wa Chama tawala na Serikali kuwa wanaweza wakawa wanajidanganya kwa kila mmoja kujibu kuwa'shabaha ya Chama, viongozi katika ngazi mbalimbaliza Chama na Serikali na wanachama; ni kuondoa umaskini wa kila mtu' kwani baadhi ya vitendo vya wahusika vinaweza vikaipotosha shabaha ya Chama.

"Najua kuwa tukiulizwa swali hili, wote tutajibu bila kusita, bila unafiki, kwamba shabaha yetu ni kuondoa umaskini wa kila mtu.Lakini tunaweza tukawa tunajidanganya, bila kutambua kuwa tunajidanganya. Baadhi ya vitendo vyetu vyaweza vikaipotosha shabaha yetu, bila ya sisi wenyewe kutambua kuwa shabaha yetu inapotoshwa," Rais wa TANU anafahamisha.

"Leo tuko Waafrika maelfu hapa Tanganyika ambao hali yetu ni nzuri sana ukilinganisha na ile ya ndugu zetu vibarua na wakulima. Na hesabu yetu itazidi kuongezeka kila mwaka. Baadhi yetu ni wakubwa wa siasa, wengine ni watumishi wa serikali kuu, au serikali za mitaa, wengine ni watumishi wa makampuni, au wanafanya shughuli zao wenyewe. Sisi wote hao tuko katika kundi la juu la Waafrika ambao hawajambo. Na mara nyingi tunayo manung'uniko mengi sana. Lakini ni mara ngapi ambapo manung'uniko hayo ni ya kutaka hali yetu, ambayo ni nzuri, ifanywe nzuri zaidi, na tofauti iliyopo sasa hivi kati yetu na ndugu zetu wa chini izidi kuwa kubwa?" Rais wa chama anatambulisha na Kuuliza.

> **Nataka kusema juu ya shida za kila siku za watu wetu.Hatuwezi tukawa kweli chama cha watu ikiwa hatujishughulishi na shida za kawaida...**



Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere

Uongozi wetu hauna budi utokane na watu wa nchi hii, bila rushwa, bila vitisho na bila ujanja wa aina yoyote. Tunapofika katika hali ya uongozi kwa kupitia mlango wa hila au rushwa, au vitisho, au ujanja wa aina nyingine yo yote, basi hatukutokana na watu wenyewe.

Asili ya pili ya uongozi wetu ni HAKI. Tuliunda TANU iondoe ukoloni pamoja na maonevu na dhuluma za aina yo yotezilizo ambatana na ukoloni. Lakini HAKI ni HAKI kwa WATU, siyo kwa majani au mitiwalinzi wa HAKI za WATU ni watu wenyewe.

Nataka kusema juu ya shida za kila siku za watu wetu.Hatuwezi tukawa kweli chama cha watu ikiwa hatujishughulishi na shida za kawaida za watu wetushida na matatizo na furaha zao za kila siku.

Maganga bin Musa aliunguliwa nyumba yake jana. Wakuu wetu wa TANU wamepata habari kwamba nyumba ya Maganga bin Musa iliungua jana. Yawezekana kuwa walisikitika sana walipopata habari hiyo. Lakini kusikitika peke yake hakutoshi. Shida ya maganga bin Musa na mkewe na watoto wake haitaondolewa na masikitiko matupu ya viongozi wa TANU na wanachama wake. Shida yake itaondolewa kwa vitendo.

Wala sisemi kwamba vitendo hivyo ni kuandika barua kwa Waziri Mkuu kuomba msaada. Nasema juu ya vitendo vya viongozi wenyewe na wanachama wa TANU. Ni juu ya viongozi kumfikia Maganga bin Musa kwa haraka kadri iwezekanavyo wasikitike pamoja naye kwa taabu aliyopata. Ila hiyo haitoshi. Ni juu yao kuita mkutano wa haraka wa Halmashauri yao, wazungumze juu ya shida ya Maganga bin Musa jinsi ya kumsaidia. Hivyo, pia haitoshi.

Ni juu yao kupita kwa wanachama na watu wengine katika kijiji chaona kuwashawishi kumsaidia Maganga bin Musa katika shida yake. Hivyo, pia haitoshi. Ni juu yao kuendelea hivyo hivyo mpaka shida ya Maganga Bin Musa imeondolewa kabisa kwa jitihada hiyo ya wanachama wa TANU na viongozi wao.

TANU ndilo kundi moja katika nchi hii ambalo halina budi lijishughulishe na shida za kila mtu. Yapo makundi ya dini au madhehebu fulani ya dini. Makundi hayo mara nyingi hushughulika na shida kama hizo nilizozitaja. Lakini kwa desturi hujishughulisha na shida za watu wa dini yao au madhehebu yao. Kadhalika yako makundi ya makabila au ukoo, yanayoshughulika na shida za aina hiyo. Tukishayazungumza na kuona jinsi ya kuondoa shida hizo, hatuna budi turuditena kwa watu wenyewe kule vijijini tuzungumze upya shida hizo na jinsi tunavyofikiri shida hizo zaweza kuondolewa kama mawazo ya watu wenyewe yatakubaliana vema. La sivyo, tusikilize watu wenyewe wana mawazo gani.

Hatuna budi tuendelee na mazungumzo haya na watu wenyewe mpaka zipatikane nji za kuondoa shida zao ambazo ni zao na ni zetu pamoja. Baada ya hapo mipango itakuwa ni mipango ya raia wenyewe, siyo mipango waliyong'ang'anizwa na wakubwa kutoka juu kama ilivyokuwa kawaida ya Serikali ya Kikoloni.

Kwa njia hiyo watu wenyewe watajua jinsi ya kushughulika na wenda wazimu wachache ambao pengine watapenda kuchafua mipango ya kuondoa shida zao.

Nimesema kuwa shida za Jumuiya hazina budi zitoke vijijini. Hii ni sheria nzuri lakini si amri ya Mungu.

Mara nyingi watu wanaweza kuendelea kuishi maisha mabaya kabisa bila kujishughulisha. Wakuu wa TANU watafanya makosa makubwa kama watawaacha watu waendelee kukaa katika maisha mabaya bila kuwaamsha.

Nimesema kuwa shida za Jumuiya hazina budi zitoke vijijini. Hii ni sheria nzuri lakini si amri ya Mungu.

Mara nyingi watu wanaweza kuendelea kuishi maisha mabaya kabisa bila kujishughulisha. Wakuu wa TANU watafanya makosa makubwa kama watawaacha watu waendelee kukaa katika maisha mabaya bila kuwaamsha.

Wakoloni walituacha tulale bila kujali shida

## Uchumi

# Februari ni mwezi wa neema Mbeya

## Wamwagiwa mabilioni ya barabara, maji





Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera

**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

NI mwezi ambao utawekwa katika historia ya wakazi wa Jiji la Mbeya na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Hii ni baada ya wakazi wa Jiji hili na wapita njia, kuelezwa kwamba zaidi ya Sh. bilioni 230 zitatumika mkoani Mbeya kuboresha miundombinu ya maji na barabara.

Waziri wa Maji , Mhe Jumaa Aweso, Spika wa Bunge ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini Mhe Dkt Tulia Ackson , Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe Juma Homera waliwaongoza wakazi wa Mbeya kushuhudia utiwaji saini wa Serikali na mkandarasi wa kuleta maji kutoka Kiwira wilayani Rungwe hadi jiji la Mbeya na vitongoji vyake.

Tukio hilo lilifanyika Februari 11, 2023 na kuhudhuriwa na watu mbalimbali ambapo ilielezwa kwamba mradi huo utagharimu zaidi ya Sh bilioni 99.66. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka miwili kuanzia sasa.

Baada ya siku nne kupita, Wakazi wa Jiji la Mbeya kwa mara nyingine walishuhudia utiwaji saini wa ujenzi wa barabara ya njia nne kutoka Uyole hadi Uwanja wa Ndege wa Songwe.

Mradi huo unagharimu zaidi ya Sh bilioni 138.1 na unatarajiwa kukamilika Februari 2025.

Utiwaji saini mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya CHICO kutoka China ulishuhudiwa pia na viongozi mbalimbali wakiwamo wabunge wote wa mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe Profesa Makame Mbarawa.

### Kwa nini Serikali itoe mabilioni kwa maji

Mkoa wa Mbeya kwa miaka mingi unatajwa kama hauna shida ya maji kama mikoa mingine, lakini ukweli ni kwamba upungufu wa maji upo mkubwa.

Kwa mkoa wa Mbeya changamoto za maji zipo zaidi katika wilaya za Chunya, Mbarali, Kyela na Jiji la Mbeya. Wilaya ya Rungwe ina changamoto, lakini wilaya hiyo imebahatika kuwa na vijito vingi ambavyo vinawasaidia wananchi.

Jiji la Mbeya lina upungufu wa maji, lakini Mamlaka ya maji katika mji huo (MBEYA UWASA) inafanya kazi nzuri kuhakikisha kilichopo kila mmoja walau anapata. Hivyo kutokana na ukweli huo wa kuwapo shida ya maji, Serikali awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeamua kutekeleza mradi ambao ulibuniwa siku nyingi ili kuondokana na adha ya ukosefu wa maji katika Jiji la Mbeya.

Maji hayo sasa yanachukuliwa kutoka Mto Kiwira uliopo wilayani Rungwe hadi jiji la Mbeya na mji mdogo wa Mbalizi. Mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka miwili.

> **Jiji la Mbeya lina upungufu wa maji, lakini Mamlaka ya maji katika mji huo (MBEYA UWASA) inafanya kazi nzuri...**

### Sh bilioni 138 kuleta sura mpya ya barabara

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe Profesa Makame Mbarawa aliwaongoza wakazi wa Mkoa wa Mbeya kushuhudia utiwaji wa saini kati ya Serikali na Mkandarasi atakayejenga barabara ya njia nne, kuanzia Uyole hadi Uwanja wa Ndege wa Songwe.

Barabara hiyo ni sehemu ya Barabara Kuu ya Tanzania hadi Zambia (TANZAM) na inajengwa eneo la katikati ya Jiji la Mbeya.

### Kwa nini ni Muhimu

Ujenzi wa barabara hiyo ni muhimu kutokana na ukweli kwamba itaondoa kero mbalimbali za usafiri hususan foleni kuanzia Iyunga hadi Nanenane.

Hivi sasa kulikatisha jiji hilo ukitokea Uyole hadi Iyunga unapoelekea Zambia utatumia muda wa saa moja ambapo umbali wake ni karibu kilometa 19 tu.

Matokeo yake daladala za kutoka Mbalizi hadi Uyole zinakatisha njia kwa kuishia Mwanjelwa kutoka ana foleni. Aidha usafiri wa bajaj katika Jiji la Mbeya ndio umeshika hatamu na kusababisha kero kubwa kwa wenye magari na watembea kwa miguu.

Barabara iliyopo ilijengwa miaka ya 1980 ikiwa kwenye tuta moja la kupitisha magari mwili tu.

Kwa ujumla jiji la Mbeya kwa sasa lipo kwenye msongamano mkubwa wa watu, magari, bahaji na bodaboda, hivyo kujengwa kwa barabara ya njia nne kutalivalisha sura mpya jiji la Mbeya.

Akizungumza kwenye hafla hizo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe Juma Homera aliwasihi wananchi wa Mbeya kumkumbuka Rais wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Aidha Waziri wa Ujenzi na uchukuzi amesisitiza kwamba Rais ndiye mtoaji mkuu wa fedha na kwamba ujenzi wa barabara hiyo unafanyika kwa kibali chake. Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Spika wa bunge la Jamhuri ya Muungano, Mhe Dk Tulia Ackson amewajibu wanaokosoa vitendo vya kumsifia Rais samia kwa miradi akisema wanamsifia Rais Samia kwa sababu ndiye anayetoa fedha sasa na ana dhamira ya dhati kuongeza kasi ya maendeleo nchini.

### Wakazi wa Mbeya wanafaidikaje Sh bilioni 230

Ni ukweli kwamba fedha hizo ni kwa ajili ya kazi za ujenzi miundombinu. Bila shaka matumizi ya fedha hizo yataongeza mzunguko wa fedha mkoani Mbeya kwa njia mbalimbali.

Miongoni mwa mwa njia hizo ni kutumika kwa ununuzi wa saruji huku wageni wengi wakihitaji mahitaji muhimu kutoka kwa wenyeji. Wataalamu watapanga nyumba, watakula vyakula vya Mbeya na kupata vinywaji mbalimbali yakiwamo moja.

Hali kadhalika miradi hiyo itatoa ajira kwa vijana kadhaa wa mkoani Mbeya na pia baadhi ya magari yatakodishwa na maofisa wa kampuni za ujenzi.

Lakini faida kubwa kwa wakazi wa Mbeya ni kwamba watapata maji ya uhakika na barabara zinazopendezesha jiji la Mbeya.

### Jambo lakufanywa na Wakazi wa Mbeya

Muhimu ni kwa wakazi wa Mbeya kuendeleza ukarimu wao na kushirikiana na wageni wanaotekeleza mradi huo.

Wadokozi , wezi na wahujumu mali za miradi wasiwepo. Bila shaka vyombo vya dola vimejipanga vema chini ya Kamanda wa Polisi Mkoa, Benjamin Kusaga .

# Biashara



# Uza sana kuliko kununua

Na Paul Mng'ong'o

NI vizuri utambue kuwa maishani mwako, lazima kuna mambo mawili yanaendelea. La kwanza ni kuuza na la pili ni kununua.

Watu wengi wa kawaida na maskini, wamekuwa hivyo si kwa bahati mbaya, bali ni kwa sababu hawana chochote cha kuuza bali wananunua zaidi.

Mafanikio si bahati peke yake (ingawa bahati ni jambo la maana). Ukitaka kufanikiwa njia ni moja tu, lazima uwe na bidhaa ya kuuza na si tu kuwa na bidhaa, bali kuiuza na ikanunuliwa.

Wengi wamejua umuhimu wa kuwa na bidhaa, lakini hazina umuhimu au ubora sokoni, hivyo hazinunuliki.

Ukitaka kufanikiwa kwenye maisha, lazima uuze kitu. Mfano:-

1. Uza tabia yako, watu waipende. Unaweza kuwa na tabia, lakini hakuna anayeipenda. Hutafanikiwa kwa tabia mbaya ambayo hakuna anayekupenda.

2. Uza mienendo yako watu waipende. Kununua kwao ni kufurahia na kukupa kibali.

3. Uza maneno yako. Unaongea nini? Unapoongea lazima watu wavutike kuongea nawe sababu unaongea busara kwa unyenyekevu. Utaona wengi wanavutwa nawe.

4. Uza utu wema, kuwa mtu wa msaada, husika vizuri na maisha ya watu nakadhalika.
Haya manne ni msingi (fundamentals), tunaita bidhaa za ndani ambazo hujengwa kwenye `package' moja inayoitwa "haiba".
Ukiuza hizi na watu wakazipenda, tayari unakuwa umetengeneza kile wanaita utajiri wa watu, jambo ambalo ndilo msingi wa vitu vingine kuja na kukupa faida.
Baada ya msingi huu (intrinsic), sasa suala la kuuza vitu kwa kipato cha kifedha (for financial gain) linafuata:-

5. Uza nguvu zako (labour), hapa ndipo tunaita kufanya kazi kwa malipo (ajira). Jitahidi kutoa nguvu zako na kufanya kazi kujipatia kipato.

6. Uza maarifa - Tafuta maarifa, wape watu wengine. Utafanikiwa.

7. Uza bidhaa - Hapa panahitaji tafiti kwanza. Angalia uhitaji wa kitu kwenye eneo moja. Nenda mahali wanauza bidhaa hiyo kwa bei ya chini kisha kauze kwenye uhitaji kwa bei yenye faida kidogo ili kutengeneza mzunguko.

8. Uza utaalam - Kuna watu wanafanya majukumu yao, lakini kuna mahali wanakwama. Peleka utaalam kama "consultant" wasaidie.

9. Uza uratibu (coordination) - Wengine hapa mmepewa uwezo wa kuratibu mambo. Nenda mahali jitangaze. Ndipo tunapata washereheshaji na waratibu (MCs) wanalipwa fedha nyingi ili kuratibu.

10. Uza huduma - Zipo huduma mbalimbali unaweza kutoa na ukapata kitu. Huduma hizi lazima zilenge kutatua changamoto fulani katika eneo husika.

11. Uza ufundi na utaalam

12. Uza ujuzi

13. Uza uwezo.

14. Uza kipaji

15. Uza burudani

16. Uza mipango - kuna watu wanauza mipango (planners).

17. Uza ubunifu - watu wanachora, wanachonga, wanabuni vitu nakadhalika.

18. Uza karisma - Mfano wanasiasa wanauza ushawishi tu. Anakuwa na maneno ya kumfanya asikilizwe na kufuatwa na makutano.

> **Yule mwanasiasa anayeuza ushawishi wake, ninyi wote mnaosikiliza, mnalipia muda wenu, kura zenu na `support' yenu ila yeye kauza ushawishi...**

Wewe unauza nini kwenye maisha yako? Au unanunua tu kila siku? Ukiwa mtu wa kununua tu, hutafanikiwa.


Yule mwanasiasa anayeuza ushawishi wake, ninyi wote mnaosikiliza, mnalipia muda wenu, kura zenu na `support' yenu ila yeye kauza ushawishi.

Si kila unachouza, kitakupa fedha. Hivyo hakikisha unauza na ununue vitu vya maana. Usinunue story za udaku mara nyingi kwa gharama kubwa ya kulipia muda wako. Usidhani unasoma udaku Instagram au ticktok bure, fahamu kuwa unalipa kwa muda wako, bando nakadhalika.

Jiulize hapa nilipokaa nauza au nanunua?

Watu wengi wana muda, lakini wanautumia muda wetu kununua nini? Tumia gharama ya muda wako kununua maarifa. Hapo kwa namna nyingine, utakuwa nawe unauza muda wako kwa ujira wa kupata maarifa. Hapo ni wewe unauza sababu unachokipata ni cha thamani.

Hapa unaposoma makala hii ndogo itakayobadilisha maisha yako maana yake unauza muda wako wa thamani kwa ujira wa maarifa haya muhimu yatakayokusaidia kubadili maisha yako.


MAMA KAZINI
Hureeee.... asante Mama kwa kutuletea umeme
ASANTE MAMA
Katuniz
KIMWELEKEO
@Muhidini Msamba
+255656122770
Wadudu wa hatari tutakuwa tunawaona kwa urahisi kwa sababu ya mwanga wa umeme
Shule
Watakuwa wanaona aibu
He! kulikoni
Utamu wa umeme kijijini kwetu babu weee...
Mama kaupiga mwingi sana kwa kutukumbuka wananchi wa huku sasa kila kijiji kitakuwa ng'ari ng'ari kwa kuwaka umeme
Ufaulu wa watoto wetu utaongezeka sana kwani watakuwa wanajisomea hadi usiku, tumuombee dua kwa Mungu ampe maisha marefu Mama yetu Rais Dr Samia Suluhu Hassan
Wamama zetu wataondokana na shida ya kutwanga nafaka kwani hata mashine zitaletwa vijijini
Wauza pombe walikuwa wanatukata sana chenji zetu sasa tutakuwa tunaziona
Huyu anaongea nini kama hamna pointi si muache kuchangia maoni
kila mtu ana uhuru wa kuchangia maoni
kwani hapa mjengoni
umeme mtamu jamani, mimi jana wacha nizime na kuwasha kama mara kumi

# Hizi ndizo fursa nzuri za kufanikiwa kibiashara

**Na Mwandishi Wetu**

NI maono ya kila familia kufanikiwa katika maeneo mengi na hususani eneo la uchumi.

Mafanikio ya kiuchumi yameumiza familia nyingi au niseme yameumiza vijana wengi; hasa baada ya kuwekeza fedha na muda wao kwenye biashara ambazo hazikuleta matunda waliyayotegemea.

Ili kubaini maeneo yenye nafasi kubwa ya kutimiza ndoto uliyonayo ya kumiliki biashara, fuatana na mwandishi wetu anayechambua fursa za kibiashara zinazotajwa kufanya vizuri.

**1. UZALISHAJI WA BIDHAA ZA LISHE**

Tanzania inatajwa kuwa na tatizo la utapiamlo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano ikielezwa kuwa asilimia 32 ya watoto wanakabiliwa na tatizo hilo. Inaelezwa kuwa mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula, ndiyo yenye tatizo kubwa zaidi.

Takwimu za mwaka huu zinaiweka Iringa kileleni mwa mikoa inayokabiliwa na utapiamlo kwa asilimia 56.9 ikifuatiwa na Njombe yenye asilimia 50 kwa ukubwa wa tatizo hilo.

Hii ni habari mbaya kwa ukuaji wa watoto, lakini ni fursa kwa watu wanaotafuta kukuza kipato na kuinuka kiuchumi.

Inaelezwa kuwa ikiwa mtu ataamua kuwekeza vyema kwenye eneo la mnyororo wa thamani kwa ajili ya chakula cha watoto na lishe kwa ujumla, ni wazi kwamba atapata wateja.

Hii ni biashara inayoweza kupata soko si Tanzania pekee, bali Afrika kwa kuwa takwimu za mwaka jana za Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), zinaonyesha kwamba takribani watoto milioni 10 wanakabiliwa na utapiamlo.

Kwa mujibu wa ripoti ya Hali ya Dunia ya Usalama wa Chakula na Lishe ya mwaka jana, idadi ya watu duniani kote ambao hawawezi kumudu lishe bora, imeongezeka hadi bilioni 3.1, hali hii inatajwa kusababishwa na kupanda kwa bei za vyakula, mabadiliko ya tabia nchi na janga la Uviko -19.

Takwimu zaidi kutoka Kituo cha Biashara cha Kimataifa kinataja eneo la lishe barani Afrika kama sehemu inayoweza kuzalisha mabilionea huku afya ya jamii ikiimarika.

Takwimu za kituo hicho zinaonyesha kwamba Afrika inaagiza vyakula vya watoto wachanga vyenye thamani ya Euro milioni 570 ambazo ni takribani Sh. trilioni 1.5 kwa mwaka na kwamba uhitaji utaongezeka zaidi hadi kufikia Sh. trilioni mbili mwaka 2026.

Tanzania ambayo imebarikiwa kuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha vyakula kuanzia nafaka hadi matunda, mboga mboga hadi maziwa, maji na rasilimali watu; ina nafasi kubwa ya kufanya vizuri katika eneo hili kwa kuwa uwekezaji huo utaokoa uharibifu wa vyakula unaotokea baada ya kuvunwa.

Hapa inahitaji mwekezaji atakayetumia teknolojia rahisi na nafuu ili ashindika chakula chenye ubora na kuuza kwa bei nafuu.

**2. UKUAJI WA TEKNOLOJIA**

Dunia imeshahamia kwenye teknolojia. Ni wazi kwamba ukitaka kuangalia fasheni za urembo, mitindo, kilimo, biashara, siasa na karibu kila kitu, unaweza kupata taarifa zake wakati wowote almradi tu una mtandao wa intaneti.

Hii ni fursa kubwa ambayo inatajwa kuwa na nafasi ya kutengeneza mabilionea. Wataalam wa biashara wanataja eneo la kilimo bado halijaguswa vyema na teknolojia.

> **Takwimu zaidi kutoka Kituo cha Biashara cha Kimataifa kinataja eneo la lishe barani Afrika kama sehemu inayoweza kuzalisha mabilionea huku afya ya jamii ikiimarika.**

Wanaeleza kuwa mtu atakayeamua kutengeneza mfumo utakaowaunganisha wakulima na wasambazaji wa pembejeo, wenye matrekta, wenye maghala ya kuhifadhia mazao, wadau wa kilimo ikiwamo serikali, masoko na hata walaji wa mwisho; umaskini unakuwa historia kwenye maisha yake.

Teknolojia kwenye eno hili inahitaji ubunifu mkubwa kwa kuwa mfumo tegemewa utakulazimu kila mtumiaji kupata taarifa hata akiwa nje ya intaneti. Mathalani, si kila mkulima anaweza kuwa na simu janja, mfumo unapaswa kuweka mazingira ya mkulima huyo kupata taarifa za bei ya mbolea, mbegu, ghala, soko, magonjwa au hali ya hewa akiwa popote kwa njia rahisi na nafuu.

Hapa limeguswa eneo moja tu la kilimo na tena kwa sehemu ndogo, yapo maeneo mengi yanayoweza kutengeneza mabilionea kuanzia kwenye sekta ya afya, mazingira, urembo, mitindo, elimu, nishati, madini, maji, utalii, ajira, vyakula, ujenzi na hata burudani.

Wataalam hao wanatoa mfano wa teksi mtandao unavyorahisisha usafiri mjini na kueleza kuwa inawezekana pia kuwa na uwezo wa kupata trekta au combine harvester mtandaoni.

**3. MABADILIKO YA TABIANCHI**

Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri karibu kila sekta duniani na wataalam wa mazingira wanaeleza kuwa ni fursa na ufadhili mwingi umeelekezwa kwenye kupunguza athari badala ya kukabili.

Jukwaa la Uchumi Duniani linaitaja sekta binafsi barani Afrika kwamba ina jukumu la pekee kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yanayoongeza majanga ya asili kama mafuriko na ukame. Jukwaa la Dunia la Uchumi linaeleza kuwa kujikita kwenye eneo hili ni dau la kushinda kwa wawekezaji barani Afrika.

Linaeleza kuwa kuwa kuna fursa za kuokoa mazingira zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 300 kwa mwaka kuanzia sasa hadi ifikapo mwaka 2030.

Uwekezaji ambao unaendelea kufanyika kwenye eneo hili ni ule wa kubuni mbinu za kilimo cha kisasa na teknolojia rahisi kwa wakulima. Lengo hapa ni kuongeza uzalishaji wa chakula ili kukabili janga la njaa linalosababishwa na hali mbaya ya hewa kama ukame au mafuriko.

Kingine kinachoweza kufanyika ni kubuni mbinu zinazostahimili hali ya hewa katika sekta muhimu za maji, nishati na udhibiti wa taka.

Mathalani, uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya kilimo au matumizi ya nyumbani na utengenezaji wa nishati mbadala kama gesi kwa kutumia mabaki ya chakula; ni eneo ambalo linatazamwa na wafadhili wanaotaka mawazo ya kuweza kuokoa mazingira kwa sasa.

Usindikaji na hususani ukaushaji wa matunda na mboga mboga kwa kutumia nishati ya jua utapunguza uharibifu wa chakula na kuongeza thamani ya mazao kwa wakulima.

Eneo lingine linaloweza kutazamwa na mtu anayejikita kwenye kuokoa mazingira ni uchumi wa kijani kama kilimo cha miti au ufugaji wa nyuki.

Elimu ya jinsi ya kukabili taka, upandaji wa miti, uvunaji wa maji ya mvua, utunzaji wa maji, nishati safi na usafi wa mazingira; ni eneo muhimu mno katika kupata ufadhili wa kutekeleza miradi hii na kisha kujenga biashara kubwa.

Fursa ni nyingi, lakini kwa leo chukua hizo tatu uone wapi unaweza kujikita na kuagana na umaskini huku ukiiokoa dunia.



# Urusi ilivyokwama kuteka eneo la Kusini mwa Ukraine

**KYIV, Ukraine**

IKIWA ni mwaka mmoja tangu Urusi iivamie Ukraine kivita, wachambuzi wanaeleza kushindwa kwa mpango wa Urusi katika vita hivyo.

Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), limezungumza na watu kadhaa nchini Ukraine ambao wameeleza mkwamo huo wa Urusi.

Uchambuzi wa BBC unaeleza kuwa, ndani ya siku chache baada ya uvamizi, wanajeshi wa Urusi waliokuwa wakishambulia kutoka Crimea, walikuwa wameteka eneo la Ukraine lenye ukubwa kuliko Uswizi.

BBC inaeleza kwamba, Februari, mwaka jana, Katibu wa Baraza la Usalama la Ukraine, Aleksey Danilov, alipokea faili jekundu lenye taarifa zilizoeleza hatari iliyokuwa ikimkabili Rais Volodymyr Zelensky.

Alisema Ukraine ilipata taarifa za uvamizi huo na Urusi ilipanga kuvamia siku mbili kabla ya tarehe iliyokuwa imetajwa.

> **Uchambuzi wa BBC unaeleza kuwa, ndani ya siku chache baada ya uvamizi, wanajeshi wa Urusi waliokuwa wakishambulia....**

Wadadisi wanaeleza kuwa, ikiwa mamlaka za Ukraine zilijua mengi kuhusu mipango ya Moscow, kwa nini askari wa Kirusi waliweza kuingia katika eneo la Kherson lililo kusini haraka hivyo?

Uchambuzi huo unaeleza kuwa, pamoja na uwezo wa majeshi ya Urusi, maandalizi hafifu ya Ukraine juu ya uvamizi, yamefanikiwa pia kuzuia nguvu za Jeshi la Moscow.

**BBC.**



Mgombea Urais kwa tiketi ya chama cha Labour, Peter Obi, akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi kabla ya kupiga kura katika kituo cha Amatutu. (PICHA: CNN).

# Ni Tinubu au Atiku Urais Nigeria

**LAGOS, Nigeria**

MGOMBEA wa Urais wa chama tawala nchini Nigeria, Bola Tinubu, anaongoza kwa kura katika majimbo 20 kati ya 36.

Hata hivyo, mgombea wa upinzani, Peter Obi, anaongoza katika Jiji la biashara la Lagos. Matokeo hayo ya awali, ni yaliyokusanywa na Shirika la Habari la Uingereza, Reuters.

Taarifa kutoka nchini humo zinaeleza kuwa, vyama vya upinzani vimesusia zoezi la kuhesabu kura vikidai kuna vitendo vya udanganyifu.

Matokeo ya awali kwa ngazi ya majimbo kutoka kwa Tume ya Uchaguzi yanaonyesha Tinubu wa chama tawala cha All Progressives Congress (APC), anaongoza kwa asilimia 39.7 sawa na kura milioni 5.4, dhidi ya Atiku Abubakar, wa chama kikuu cha upinzani cha People's Democratic Party (PDP) anayetajwa kupata kura milioni 4.4 sawa na asilimia 32.2.

Peter Obi kipenzi cha vijana

Mgombea Peter Obi wa chama kidogo cha Labour, anashika nafasi ya tatu kwa kura milioni 2.2 sawa na asilimia 16.3.

Wachambuzi wa siasa nchini humo wanaeleza kuwa, ushindi wa Obi katika Jimbo la Lagos kwa kura 582,454 dhidi ya 572,606 kwa Tinubu, imekuwa hatua kubwa kwa mwanasiasa huyo.

Taarifa zaidi zinaonyesha kwamba takribani theluthi mbili kura hazijahesabiwa kutokana na uhaba wa vitendea kazi. Hata hivyo, vyama vya upinzani vimeonyesha kutilia shaka mwenendo wa Tume ya Uchaguzi huku mgombea Obi akieleza mchakato wa uchaguzi umevurugwa.

Akin Oshintokun, Mkurugenzi wa Kampeni katika timu ya kampeni ya Obi, ametoa wito wa Tume ya Uchaguzi wa Nigeria, kuzingatia muongozo wake, lakini kinyume chake waache kutangaza matokeo.

Meneja wa kampeni wa Atiku wa PDP, Melaye Dino, akiwa katika kituo cha kujumlisha matokeo cha Abuja, alisema jana kwamba wamepoteza matumaini na matokeo hayo.

**DW.**

# UN yachangisha fedha kuisaidia Yemen, Marekani kuongeza fungu

**GENEVA, Uswis**

UMOJA wa Mataifa umechangisha fedha kiasi cha Dola bilioni 1.2 kwa ajili ya misaada ya kibinadamu kwa Yemen iliyokumbwa na vita.

Hata hivyo, kiasi hicho ni kidogo ikilinganishwa na lengo lililowekwa na umoja huo la kukusanya Dola bilioni 4.3.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, aliuambia mkutano wa wafadhili wa kimataifa mjini Geneva mapema wiki hii kwamba, Marekani itatoa Dola milioni 444 za misaada ya kibinadamu kwa Yemen mwaka huu, na kuwataka wafadhili wengine kuongeza michango yao.

"Kiwango cha changamoto tunachokabiliana nacho kinatisha. Lakini natoa wito kwa kila mtu kuweka mtazamo wetu kwa watu tunaotaka kuwasaidia," alisema.

Blinken alisema kuwa uhaba wa fedha wa mwaka jana kwa Yemen, ulilazimisha mashirika ya Umoja wa Mataifa kupunguza operesheni nchini humo, ikiwa ni pamoja na mgao wa chakula.

**VOA.**

# Wahamiaji 61 wafa maji Italia

**ROME, Italia**

IDADI ya wahamiaji waliokufa baada ya boti yao kupata ajali Kusini mwa pwani ya Italia, imefikia watu 61.

Taarifa zinaeleza kuwa maofisa wanaendelea kuwatafuta watu wengine waliozama baada ya ajali hiyo.

Boti hiyo iliyotengenezwa kwa mbao, ilikuwa imebeba wahamiaji kuelekea Ulaya kutokea Uturuki.

Inaelezwa kwamba boti hiyo iliharibika mapema Jumapili baada ya kugonga miamba karibu na Steccato di Cutro, Mashariki mwa Pwani ya Calabria.

Hata hivyo, watu 80 wameokolewa katika ajali hiyo.

Taarifa zinaeleza kuwa boti hiyo ilikuwa imebeba watu kutoka Afghanistan, Iran na nchi nyingine. Miongoni mwa waliofariki dunia ni watoto 12.

Manusura wa ajali hiyo walieleza kuwa boti hiyo ilikuwa imebeba kati ya watu 180 na 200.

Mtu mmoja aliyenusurika kifo amekamatwa kwa kufanya biashara ya kusafirisha watu na maofisa wa polisi wa forodha walisema kwamba wanakamilisha mchakato wa kuwakamata watu wengine wawili kwa kushiriki katika kusafirisha watu kinyume cha sheria.

**VOA.**



**Karibu katika duka letu ili kupata bidhaa halisi za Chama Cha mapinduzi**

**Tunauza:**

- Kaunda suti
- Shati
- Tisheti
- Magauni
- Weel cover
- Note book
- kalamu
- viatu
- Kofia
- n.k.

**Mawasiliano**

+255 733 768 825
info@umg.co.tz
www.umg.co.tz

**Tunapatikana**

Ofisi ndogo za CCM Lumumba

Jarida la MWELEKEO

**SOMA NA PAKUA GAZETI HILI BURE**
Kupitia.

**www.umg.co.tz**


www.umg.co.tz
Mweleke0
Leo yetu ndiyo kesho yetu
AFYA
Nini kifanyike kukabili kisukari Afrika
Maajabu, mwili mmoja makaburi mawili
Dk. Samia: Vijiji vyote umeme mwaka huu
... Tundu Lissu sasa amkubali
HABARI NDANI
Undani wa Wajumbe Sekretarieti ya NEC ya CCM
Nini kitatokea Ukraine Feb. 24

@jaridalamweleko

# Carragher na maoni kuhusu mabeki wetu wa kati



**Na Mwandishi Wetu**

BEKI mstaafu wa Klabu ya Liverpool, Jimmy Carragher, ni mmoja wa wachambuzi wa Kituo cha Skysports cha kurusha matangazo ya moja kwa moja ya Ligi Kuu ya England.

Akiwa studio, hukaa pembeni ya Thierry Henry na yupo mdogo wao, Micah Richards aliyecheza soka baada ya wachezaji hao wawili kuanza kuwa na umri mkubwa.

Akiwa katikati ya uchambuzi wa mechi mojawapo ya Manchester United, aliwakumbusha wenzake kuwa kimo cha beki wa kati wa timu hiyo kutoka Argentina, Martinez, si kile alichofundishwa na makocha wake kuwa ni lazima kiwe na viwango fulani vya urefu.

Kwa ufupi, hakutaka kupepesa macho, aliamua tu kuwa mkweli kwamba, Martinez analo umbo dogo kulinganisha na kiwango cha kawaida cha mabeki wengi wa kati.

Anaweza kuwa na nguvu na stamina ya kutosha, lakini urefu wake haufanani na ule unaozoeleka kuonekana wakati mabeki wawili wa mwisho wanaposimama kwa pamoja. Hata hivyo, alipingwa na wale wanazi wa Man United kama ilivyotarajiwa.

Akiwa mchezaji wa zamani wa Liverpool, Carragher anaonekana kuwa na nia inayojificha na isiyokuwa na wema ndani yake pale anapotoa maoni ya kiuchambuzi dhidi ya Man United. Hivyo alikutana na maoni mengi yenye kumpinga japo hoja yake ya msingi ina mashiko.

Beki wa kati awe wa upande wa kulia au wa kushoto, angalau awe na urefu wenye kwenda sambamba na ule wa washambuliaji anaokabana nao kwa dakika 90 za mchezo.

Maoni ya Carragher, yamefanana na maamuzi jasiri aliyoyafanya Kocha wa Taifa Stars wa mwaka 1995, Mbrazil Clovis Oliveira, pale alipoamua kumtoa George Masatu kutoka kuwa beki wa kati na kumpeleka upande wa kulia, namba mbili. Wajuaji wa mpira hawakumuacha salama Oliveira, walimshambulia na kumtusi kwa aina zote za maneno machafu wanazozifahamu miaka ile.

Nafasi ya Masatu, ikachukuliwa na Mustapha Hoza, beki mrefu, lakini mwenye mwili mzito na asiyekuwa na ufundi mwingi wa kuuchezea mpira miguuni.

Kwa kocha huyo aliona ni heri awe na sentahafu asiye na kipaji kama Masatu, lakini mwenye urefu unaofanana na ule wa mabeki wa kati kwa viwango vya kimataifa.

Na hata miaka ile ya 2000 katikati alipokuja Mbrazil mwingine, Marcio Maximo, aliweka msisitizo katika kuwa na asilimia kubwa ya timu inayoundwa na wachezaji vijana wenye vimo virefu.

Akawa akimuandaa beki mmoja pale Mtibwa, Dickson Daud, ili awe sentahafu wa Stars kwa miaka kadhaa mbeleni.

Bahati mbaya Dickson, akapata maumivu makubwa yaliyoathiri uchezaji wake na hivyo mipango ya Maximo, ikawa imetiwa doa.

Naona kama vile Simba na Yanga, wamekumbushwa kwa vitendo juu ya timu zao kujaza wachezaji wengi wenye urefu unaokubalika kimataifa.

Simba wamekuwa wajanja miaka michache ya karibuni, hawakubali kuwa na mabeki wawili wa kati wenye vimo vya kawaida tu.

Henock Inonga Baka, atasimama na Kennedy Juma. Kennedy atasimama na Joash Onyango. Onyango atasimama na Inonga. Wote hao watatu ni mabeki wenye vimo vyenye kukubalika katika viwango vya kimataifa na pia wanaye Mohamed Outtarra, ambaye anamudu kucheza beki wa kati. Yanga wanaye beki mmoja matata sana wa kati, Dickson Job, lakini hakujaliwa katika suala la kimo.

Anakaba vizuri na anajua kutazama shambulizi linalofuatia litaelekezwa wapi (anticipation), ili ajipange sehemu gani kwa ajili ya kulizuia.

Job ni mfupi na mdogo wa umbo, ambao ulianikwa wazi wakati mpira wa kona uliopigwa kule Tunisia kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho, ulipotua katika kichwa cha mshambuliaji bonge la mtu raia wa Mali, Boubacar Traore na kufunga bila ya kusumbuliwa na mtu katika eneo la katikati.

Anapocheza na washambuliaji wengi wa kati wa Ligi Kuu, tatizo la kuwa na kimo kidogo haliwezi kuonekana. Atajipanga wakati wa mipira ya kona na ataicheza bila ya wasiwasi.

Hayupo mshambuliaji mwenye urefu wa sentimenta 195 na zaidi na mwenye kilo 80 za msuli wa mazoezi, mwenye kutegemewa kumsumbua katika kuicheza mipira ya hewani.

Na mpaka Simba kuwa na mitazamo ya kimataifa imepita chini ya makocha kadhaa wa viwango vya juu ambao hawakutaka kufanya kazi na mabeki wafupi. Pia wamekuwa wakiajiri wataalam wa kuzisoma mechi hasa zile za makundi ya Ligi ya Mabingwa, watu wenye jukumu la kuutazama uwezo na udhaifu wa timu itayaocheza na Simba mechi zinazofuata katika mtiririko mzima jinsi ulivyo wa mechi kadiri ya michuano ya msimu husika.

Hawa ni wataalam ambao lazima wanatoa ushauri kwa menejimenti juu ya kutafuta mabeki wenye sifa fulani au viungo wa aina fulani. Ikawabidi na wao kubadilika, ili waendane na falsafa za kimpira za kidunia. Tunaendelea kujifunza mengi kuhusu mpira na elimu huwa haizeeki na haina mwisho.

**Kwa ufupi, hakutaka kupepesa macho, aliamua tu kuwa mkweli kwamba, Martinez analo umbo dogo kulinganisha na kiwango cha kawaida cha mabeki wengi wa kati...**




| MANCHESTER UNITED LISANDRO MARTINEZ | | LIVERPOOL VIRGIL VAN DIJK |
|---|---|---|
| 315 | Dakika alizocheza | 360 |
| 83% | Mipira ya chini aliyoshinda | 81% |
| 9 | Mipira ya juu aliyoshinda | 4 |
| 21 | Mipira aliyookoa | 12 |
| 8 | Mipira aliyoikatiza | 4 |
| 5 | Mipira aliyozuia | 1 |

# Burudani

## R. Kelly ‘kutumikia kifungo hadi 2066’

**NEW YORK, Marekani**

MWANAMUZIKI wa R&B nchini Marekani aliyegeuka kuwa mhalifu maarufu R.Kelly inadaiwa hataachiwa hadi 2066, yaani mwaka mmoja kabla ya kutimiza miaka 100, ikiwa Jaji wa Shirikisho atakubali mapendekezo ya waendesha mashtaka katika kesi yake ya hukumu katika mji wa Chicago.



Kelly ,56, atahukumiwa kwa makosa yake kutoka mwaka jana huko Chicago ya ponografia ya watoto na ushawishi wa kingono na tayari, anatumikia miaka 30 kwa hatia zake za ulaghai na biashara ya ngono 2021 jijini New York.

Katika memo ya hukumu, walipendekeza Kelly kutumikia miaka 25 zaidi Waendesha Mashtaka walimtaja mwanamuziki huyo kama ‘mnyanyasaji wa kingono’ ambaye alitumia umaarufu na utajiri wake, kuwashawishi mashabiki wakubwa kuwanyanyasa kingono na kisha kuwatupilia mbali.



## Familia yadai Bruce Willis ana shida kiakili

**NEW YORK, Marekani**

FAMILIA ya mwigizaji maarufu nchini Marekani, Bruce Willis imedai kuwa nguli huyo wa filamu ana shida ya kiakili inayofahamika kama ‘frontotemporal.

Kwa mujibu wa taarifa kwenye mitandao ya kijamii, familia ya mwigizaji huyo ni kuwa ndugu yao ana ‘unafuu wa kupata utambuzi wazi’.

Mwigizaji huyo mwenye umri wa miaka 67, aligunduliwa kuwa na aphasia ambayo husababisha matatizo ya kuzungumza katika majira ya joto mwaka jana, lakini hali hiyo imeendelea na amepewa uchunguzi maalum zaidi. Familia iliendelea kusema kuwa shida ya akili ya frontotemporal, ndiyo aina ya kawaida ya matatizo kiakili yanayowaathiri watu walio na umri wa chini ya miaka 60.

“Mpaka sasa hakuna matibabu ya ugonjwa huo, tatizo ambalo tunatumai linaweza kutatuliwa miaka ijayo,” ilisomeka sehemu ya taarifa hiyo.

## Aliyedaiwa kumuua Hussle ahukumiwa jela miaka 60

**LOS ANGELES, Marekani**

MTU mmoja aliyekutwa na hatia ya kumuua rapa maarufu nchini Marekani, Nipsey Hussle amehukumiwa kifungo cha miaka 60 jela.



Mtuhumiwa huyo, Eric Holder Jr. alikutwa na hatia ya mauaji ya kiwango cha kwanza Julai mwaka jana kwa kosa la kumuua, Hussle ambaye jina lake halisi ni Ermias Asghedom aliyekuwa nje ya duka la nguo la Hussle Kusini mwa Los Angeles mwaka 2019.

Hussle msanii aliyeteuliwa na Grammy, alifariki akiwa na umri wa miaka 33. Watu wawili waliokuwa karibu pia walipigwa risasi na kujeruhiwa katika tukio hilo.

Jaji wa Mahakama ya Juu, Clay Jacke alitangaza kifungo cha miaka 60 hadi maisha cha mshukiwa baada ya kusikia kutoka kwa mmoja wa marafiki wa Hussle, pamoja na kusoma barua kutoka kwa baba yake Holder.

## Harmonize awapa darasa wasanii wa Bongo

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya nchini, Harmonize ameamua kutoa ya moyoni kuhusu wasanii wa muziki wa Bongo Fleva kutokua na ushirikiano, hasa kupeana sapoti ili kukuza muziki huo kimataifa.



Alitoa kauli hiyo katika ukurasa wake wa Instagram ambapo alisema, moja ya kitu kinachosababisha muziki wa Bongo Fleva kutokua mkubwa ni chuki zisizo na maana miongoni mwa wasanii.

“Hakuna kitu kingine kinachosababisha muziki wetu kushindwa kupasua anga za kamataifa zaidi wasanii kuwa na chuki binafsi,” alisema.

Alitolea mfano wa wasnaii wa Nigeria akiwataja Wizkid, Burna Boy na wengine akisema huenda wako na shughuli nyingi za muziki ndiyo maana hawagombani.

Wasanii wa Bongo Fleva wanapishana humu humu, ndiyo maana wanarushiana maneno yasiyo kuwa na msingi kwani wakitaka kufanikiwa ni lazima washikamane kama ilivyo kwa wasanii wenzao wa nchini Nigeria.

# Bajeti ya Namungo FC sasa ni bilioni 2/-

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

KLABU ya Namungo, imeziomba kampuni zilizowekeza katika sekta mbalimbali ikiwemo ya madini wilayani Ruangwa, kuidhamini timu hiyo iwe na uwezo wa kushindana na kutwaa mataji ya ndani na hatimaye, ipate nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Namungu FC inasema, ili imudu kushindana kikamilifu inahitaji sh. bilioni 2 kwa kuanzia msimu ujao, kiasi ambacho kitagharamia kambi ya mazoezi kabla ya msimu wa Ligi Kuu kuanza (pree sison), mishahara na posho za wachezaji na wataalam wa benchi la ufundi.

Wito huo ulitolewa na mlezi wa klabu hiyo, Kassim Majaliwa wakati wa halfa ya kuzindua tawi la Namungo FC la Tairi Tatu lililopo mjini hapa, ambapo alikuwa mgeni rasmi.

Majaliwa ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Ruangwa alisema, hivi sasa Wilaya ya Ruangwa ina fursa nyingi za uwekezaji hasa katika sekta ya madini, ambapo kwa sasa kuna zaidi ya kampuni 12 zilozowekeza katika migodi tofauti.

"Nimepata nafasi ya kuzindua tawi hili, lakini ni vizuri nikatumia fursa hii kuwaomba wawekezaji na wafanyabishara mmoja mmoja kuidhamini Namungo FC, ili timu yetu iwe na uwezo wa kiuchumi ili ishindane kikamilifu na wapinzani," alisema.

Majaliwa ambaye pia ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alisema Namungo FC inahitaji udhamini kwa udi na uvumba ili msimu huu imalize ikiwa katika nafasi nne za juu ipate nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa.

Alisema kwa kufanya hivyo timu zote za ndani na nje ya nchi, zitakuja Ruangwa na kucheza na Namungo kwenye Uwanja wa Majaliwa.

Kwa sasa Namungo inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC ikiwa na alama 29 baada ya kucheza mechi 24, ambapo Mwenyekiti wa tawi la Namungo Tairi Tatu, Shedafa Mandia, aliwataka wanachama wa matawi mengine wilayani Ruangwa kuunganisha nguvu ili kuisaidia timu yao ifanye vizuri.

# Wachezaji walio tayari waandaliwe muda huu

**Inatoka Uk.24**

Tunajaribu kuwachukua wachezaji vijana wawili watatu na kuongozana nao katika safari za vikosi vya kwanza, lakini Sasa hivi akili za Wanayanga na Wanasimba zimeelekezwa katika kutafuta pointi za mechi za Ligi ya Mabingwa na zile za Kombe la Shirikisho.

Kila Mwanasimba anawazia pointi sita za nyumbani kwamba zitaipa timu pointi tisa, zitakazoiwezesha kuvuka hatua ya makundi na kusogea robo fainali.

Kinachoendelea miongoni mwa Wanayanga ni kuiombea dua njema ishinde mechi za ugenini kule Mali na DRC. Lakini huko wanapocheza hizo mechi, kuna mazingira mazuri sana ya kupata wachezaji wenye uwezo wanaopitia katika mfumo wa soka la vijana.

Isiwe tu ni safari za kutafuta pointi tatu ili timu zisogee juu katika misimamo ya makundi yao. Ziwe pia ni maalum kwa kutafuta wachezaji kadhaa wanaoweza kuziba mapengo ya timu zao yanayojionesha wanapocheza mechi ngumu za kimataifa.

Waende huko wakiwa na nia mbili, ya kwanza kutafuta pointi tatu na ya pili iwe ni kufanya utafutaji (scouting) wa wachezaji wanaofiti katika mahitaji ya makocha ya kuimarisha vikosi vya kwanza.

Ukimuangalia, Othman Pape Sakho ni mshambuliaji kijana aliyepitia katika misingi halisi ya kimpira. Na alikuja Simba akiwa ni kijana mdogo wa chini ya miaka 25.

Katika umri aliokuja nao Tanzania na machachari yake ya uwanjani, sidhani kama kuna kijana wa Kitanzania wa rika lake mwenye uwezo wa kuwa ndio vichwa vya habari vya magazeti ya mataifa mengine ya Afrika.

Na huko Senegal hawana kabisa taarifa za kina za Sakho. Nina uhakika walianza kumfahamu baada ya kufunga goli bora la michuano yote ya CAF msimu uliopita.

Wanao wachezaji wengi vijana, wanaotamba Ulaya yote achilia mbali hawa wanaokwenda huko na kurudi barani Afrika.

Kukomaa kwa Sakho, mpaka akaja kuwa mchezaji wa kikosi cha kwanza tena anayetoka nchi nyingine ni mtihani halisi tunaotakiwa kuufikiria kuliko hizi ndoto za kuvuka hatua ya makundi ya CAF.

Tunayo Simba yenye ushawishi mpaka wa kuingiza timu katika michuano maalum ya Super Cup, lakini tunakuwa na timu zisizo na muendelezo wenye kueleweka. Soka la vijana ni suluhisho la timu kuwa na vikosi vyenye muendelezo unaoeleweka.

Na utafutaji wa wachezaji ukifanywa kwa usahihi mchezaji wa aina ya Ismael Sawadogo, hawezi hata kupanda ndege kuja kucheza Simba wakati hajacheza mpira msimu mzima uliopita huko alikotoka.

Tunapenda sana wachezaji waliopikwa na vyanzo tofauti vya mataifa mengine mpaka tunasahau kuwa walichokifanya hata sisi, tuna uwezo wa kukifanya kama tukiweka umakini katika mpira wa kisasa.

Sifa za timu kuwa ndani ya zile kumi na tano bora kwa viwango vya CAF ni za muda tu. Timu inaweza kupotea na kutoka katika orodha hiyo kirahisi kama hakuna mwendelezo wa usimamiaji wa soka la vijana kisayansi unaotiliwa mkazo.

Simba ina wachezaji walioanza kuwa sehemu ya kikosi cha kwanza tangu msimu wa 2018 ni dhahiri kasi yao imeanza kupungua. Kuendelea kuwaamini na kuwategemea ni lazima kuje na matokeo ya kukera katika baadhi ya mechi za kimataifa.

Ni wachezaji waliotumika sana na kwa sasa akili zinataka kufanya kitu lakini miili imeanza kukataa. Timu kama Raja, Wydad, Al Ahly na Mamelodi zina muendelezo mzuri wa vikosi vyao.

Hawapati shida kujua fulani na fulani wakianza kuchoka ni nani watakaokuwa warithi wao. Yanga na Simba watafute ufalme wa mpira wa Afrika wakijua kuwa ipo hiyo changamoto.

# Droo michuano ya Kombe la FA kufanyika Machi 4

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Kamati ya Mashindano ya Kombe la Shirikisho la Zanzibar 'FA', Ali Bakari Cheupe amesema upangaji wa ratiba kwa ajili ya hatua ya pili ya mtoano wa kombe hilo inatarajiwa kufanyika Machi 4 mwaka huu, ambapo mechi hizo zitaendelea tena Machi 16 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Ukumbi wa Mikutano wa Shirikisho la Mpira Zanzibar ZFF), Cheupe alisema tayari wameshatoa barua kwa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya ligi kuhusu kuzijulisha timu 14 za Unguja za Ligi Kuu na Makatibu wa Vyama vya Mpira vya Mikoa kwa ajili ya kuzijulisha timu zao, zilizofanikiwa kuingia hatua ya pili na kuanza kujiandaa kwa ajili ya zoezi la upangaji wa ratiba hiyo.

Alisema kwa upande wa Pemba wamemjulisha Naibu Katibu Mkuu wa ZFF kisiwani humo kuzijulisha timu mbili za Ligi Kuu na za Daraja la Kwanza na zile za mikoa, ambazo zimefanikiwa kuingia katika hatua hiyo ya pili. Aliztja timu ambazo zimetinga hatua ya pili ya michuano hiyo katika kisiwa cha Unguja zinazocheza Daraja la Kwanza ni New King, Raskazone, New City, Jang'ombe Boys, New Boys, Mundu, Umoja wa Mbuzini na Mwembe Makumbi City.

Kwa upande wa klabu za mikoa ambazo zimefikia hatua hiyo ya pili ni Bambuu FC, Mwembe Ladu, Villa FC, Muungano Rangers, Kiembe Samaki, Nyagobo, Baharia FC, Sharp Boys, Mwembe Makumbi United na Danger Boys.

Kwa kisiwa cha Pemba, timu zilizofanikiwa hatua hiyo ukizitoa Jamhuri na Chipukizi timu za daraja la kwanza zipo Kisiwani FC, Mkoroshoni, Maendeleo United, FFC, New Stone Towne, Al-Azaar, Macho Mane United, Tekeleza FC, Junguni FC na Young Islanders.



Mshindi wa mbio za Tigo Kili Half Marathon, Emmanuel Giniki akimaliza mbio hizo zilizofanyika mjini Moshi mwishoni mwa wiki. Na Mpigapicha Wetu

# SMZ: Baadhi ya viwanja vya soka haviridhishi Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar 'SMZ), imekiri kwamba baadhi ya viwanja ambavyo hutumika kwa shughuli za michezo Zanzibar kuwa haviridhishi.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea visiwani hapa wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Dimani, Mwanaasha Khamis Juma.

Waziri Tabia alisema, Wizara inafanya jitihada kubwa kutatua changamoto hiyo angalau kwa kuanzia na viwanja vya wilaya.

Alisema kupitia bajeti ya serikali na fedha za wahisani, wataendelea kuboresha na kujenga miundombinu ya michezo Unguja na Pemba.

Hata hivyo alisema kwa sasa, viwanja vilivyopo katika Jimbo la Dimani havimo katika mpango huo wa kuviboresha wanaoendelea nao.

"Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza awamu ya kwanza ya mpango huu, wizara inaweza kujiridhisha na kufanya mazungumzo na wamiliki wa viwanja hivyo na endapo tutakubaliana, basi wizara haitasita kuviboresha ili vijana wacheze mpira katika mazingira mazuri," alisema Waziri Tabia.

Mwakilishi huyo katika suala hilo, alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kusaidia kuviendeleza moja ya uwanja ulichoko katika jimbo lake, angalau kwa kuweka miundombinu mizuri ikiwemo nyasi bandia.



## R. Kelly 'kutumikia kifungo hadi 2066'

Uk. 22

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Mwelekeo Spoti

| Jumanne Machi 1 Machi 7, 2013 |



## Bajeti ya Namungo FC sasa ni bilioni 2/-

Uk. 23

# Wachezaji walio tayari waandaliwe muda huu

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU zetu ni kama zinaugua ugonjwa wa kupenda kuona mchezaji aliye tayari ndiye akiwa anaanza kila mechi.

Ni ugonjwa wa miaka na miaka haijulikani ni lini dalili zake zilianza kujionesha hadharani.

Hatupendi wala hatuwezi kuvumilia kuyaona makosa ya mchezaji mwenye umri mdogo akiwa anacheza mechi zake za awali ndani ya jezi ya Yanga au Simba.

Yanga ya Profesa Nasreddine Nabi wanamvumilia Clement Mzize. Sababu ni moja tu, wanayo timu nzuri yenye ubingwa mkononi wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara msimu uliopita.

Na kuna mwenendo mzuri wenye kuashiria kubeba tena taji hilo. Tofauti ya pointi nane iliyopo kati yao na Simba haiwapi aina yoyote ya presha.

Wanashangilia mechi wakiwa na furaha hata kama matokeo yanamalizika kwa sare ya mabao au ile tasa ya 0-0. Nafasi ya Mzize kuwa uwanjani haiwasumbui vichwa wanachama na mashabiki.

Jaribu tu kujiuliza kama Yanga, ingekuwa haijabeba taji msimu uliopita na vita ya ubingwa msimu huu ingekuwa haieleweki.

Sidhani kama Mzize, angekuwa na nafasi ya kucheza kwa uhuru na furaha. Huu ni muda wa kufanyia kazi makosa ya wachezaji wanaokuwa kiuwezo.

Ni muda wa kuvumilia kile wanachokosea hata baada ya kufundishwa kwa kina katika uwanja wa mazoezi. Hatuna kabisa utamaduni huu.

Inaendelea Uk.23



# Kocha Mgunda amzungumzia Kibu Denis

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Msaidizi wa Klabu ya Simba amemzungumzia mshambuliaji wa timu hiyo Kibu Denis, ambapo amesema ni mchezaji mpambanaji asiyekata tamaa uwanjani muda wote.

Licha ya Mgunda kumpa tano mchezaji huyo baadhi ya mashabiki wa timu hiyo ambao mara kadhaa walikua wakimkosea kutokana na kukosa kwamba anakosa mabao ya wazi kila anapopata nafasi ya kucheza.

Akizungumza mara baada ya timu yake kupata ushindi wa bao wa 1-0 dhidi ya Vipers wikiendi iliyopita katika mechi ya Klabu Bingwa Afrika iliyochezwa nchini Uganda, Mgunda alisema siku zote Kibu, anapopata nafasi ya kucheza huwa anajitoa kwa kiasi kikubwa na kuweza kuisaidia timu yake kupata matokeo.

Alisema katika mechi hiyo alichangia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa ushindi huo wa bao 1-0 na kuifanya Simba kufufua matumaini ya kuweza kucheza robo fainali ya michuano hiyo.

"Kwa kiasi kikubwa Kibu Denis huwa anaisaidia timu kwa kiasi kikubwa, ukiangalia hata katika mechi yetu ya Ligi Kuu dhidi ya Azam FC yeye ndiye alichangia kupata sare ya bao 1-1," alisema kocha huyo.

Akizungumzia mchezo dhidi ya Vipers, Mgunda alisema ulikuwa mgumu kutokana na mazingira waliyokuwa nayo awai kwani walikuwa hawana pointi hata moja katika michuano hiyo.

Alisema anajua mashabiki wao walikuwa wako katika wakati mgumu baada ya kupoteza mechi mbili za michuano hiyo, lakini anawahakikishia mashabiki hao watapigana ili kuweza Ushindi huu umeturudisha katika resi za kuweza kwenda kucheza robo fainali hivyo tutapigana hadi tone la mwisho kuhakikisha tunasonga mbele," alisema Kocha Mgunda.

Wawakilishi hao wa Watanzania kwenye mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Jumamosi watarudiana Vipers ya Uganda katika mechi itakayopigwa Uwanja Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam.



Kibu Denis